# Nipashe

Jumatatu Agosti 3, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580300

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Serikali yanasa w'biashara sugu utoroshaji madini nje

UKURASA 3




UKURASA 11




Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe (wa tatu kushoto), akiendesha kikao cha Kamati Kuu ambacho kilifanya utafiti wa majina ya wagombea wa urais na wagombea wenza ambayo yatawasilishwa Baraza Kuu leo. Wengine kutoka kushoto ni Makamu Mwenyekiti (Zanzibar), Said Issa; Makamu Mwenyekiti Bara, Tundu Lissu; Katibu Mkuu, John Mnyika; Naibu Katibu Mkuu (Bara), Benson Kigaila na Naibu Katibu Mkuu (Zanzibar), Salim Mwalimu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Jina mgombea urais CHADEMA hadharani kesho

• **Ni** baada ya vikao vya juu jana na leo kuwachuja watiania, yafafanua ugombea wa Lissu, wa ACT-Wazalendo kujulikana... *Endelea Uk. 2*


## FURSA KWA WAGOMBEA!




Gazeti la Nipashe linatoa fursa kwa wagombea wote wa vyama vya siasa kunadi sera zao kupitia kurasa zetu kwa gharama nafuu.

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi
The Guardian Limited
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz


## Mchujo CCM utakavyokuwa walioongoza kura

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** AZAM YAIPIKU YANGA KWA NIYONZIMA UK.23 | **MAONI, KATUNI** UK.6



Wasimamizi wa uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba wa mikoa ya Shinyanga na Simiyu, wakila kiapo cha utii katika kusimamia vizuri uchaguzi huo wa kuchagua madiwani, wabunge na rais, ili ufanyike kwa haki. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Jina mgombea urais CHADEMA kesho

**Na Waandishi Wetu**

WAGOMBEA wa nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wanatarajiwa kujulikana kesho.

Wagombea wa nafasi hiyo Bara na Zanzibar watajulikana baada ya Kamati Kuu ya chama hicho kuanza kujifungia toka jana kupitia na kujadili majina ya wagombea waliotia nia katika nafasi hiyo.

Jana kamati hiyo ilianza vikao vyake vya mchujo ambavyo vinafanyika kwa siku tatu mfululizo.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa chama hicho, Tumaini Makene, Kamati Kuu ilianza kutafiti majina ya wagombea hao jana, na leo watapigiwa kura na baadaye yatawasilisha kwa Baraza Kuu la chama hicho ambalo linaketi leo.

Makene alisema majina yanayotakiwa kupigiwa kura leo ya wagombea urais ni wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na mgombea mwenza na mgombea wa nafasi hiyo ya urais upande wa Zanzibar.

Makene alisema baada ya Baraza Kuu kupitisha majina ya wagombea hao kwa Jamhuri na Zanzibar, yatakabidhiwa kwa Katibu Mkuu wa chama hicho leo ambaye naye atayawasilisha katika Mkutano Mkuu utakaofanyikia kesho kwa ajili ya uamuzi wa mwisho.

"Kamati Kuu leo (jana), ilifanya utafiti wa kupata majina ya wagombea nafasi ya urais ya wa Jamhuri na mgombea mwenza pamoja na mgombea wa nafasi hiyo Zanzibar," alisema Makene.

"Na itawasilisha majina hayo kwenye Baraza Kuu la Taifa la chama leo ambalo nalo litapendekeza majina hayo na kuyawasilisha kwa Katibu Mkuu wa chama."

Makene alisema pamoja na kujadili majina ya wagombea urais, pia Kamati Kuu hiyo ilijadili ilani ya uchaguzi ya chama hicho ambayo nayo itapitishwa kesho.

Jumla ya watiania saba ndiyo waliorejesha fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea nafasi hiyo ndani ya CHADEMA akiwamo Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu, mwingine ni aliyekuwa Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita, Wakili Simba Neo, Leonard Manyama, Gasper Mwanalelya, Lazaro Nyalandu na Dk. Maryrose Majinge.

**ACT-WAZALENDO JUMATANO**

Wakati huohuo, Chama cha ACT-Wazalendo, kinatarajia kuwatangaza wagombea wake wa urais wa Muungano na Zanzibar keshokutwa.

Akizungumza waandishi vya habari jijini Dar es Salaam jana, Naibu Katibu Mkuu wa Idara ya Habari na Uenezi wa chama hicho, Janeth Rithe, alisema Kamati Kuu ilikutana jana kuyachambua majina hayo.

Alisema Halmashauri Kuu itakutana leo ikifuatiwa na Mkutano Mkuu, yote ikiwa na lengo la kutangaza ilani ya chama na wagombea urais kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.

"Tutakuwa na jambo la kwanza la kupata mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini mgombea urais kwa upande wa Zanzibar na lingine ni uzinduzi wa ilani yetu ya uchaguzi, alisema Rithe.

**USHIRIKIANO NA VYAMA**

Akizungumzia suala la muungano wa vyama ili kupata nguvu ya pamoja kuelekea uchaguzi huo, Rithe alisema jambo hilo bado lipo kwenye hatua ya mazungumzo kwa kuwa linahusisha mambo mengi.

"Tukizungumzia suala la ushirikiano bado lipo kwenye mazungumzo, ushirikiano si hitaji tu la vyama ni hitaji pia la wananchi," alisema Rithe.

**Imeandikwa na Elizabeth Zaya na Enock Charles**

# Mchujo utakavyokuwa walioongoza kura CCM

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

MCHAKATO wa kuwapata wagombea wa nafasi za ubunge, uwakilishi na udiwani ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ulisitishwa kwa muda kupisha maombelezo ya kitaifa kufuatia kifo cha Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa.

Baada ya maziko ya kiongozi huyo yaliyofanyika Lupaso wilayani Msasi mkoani Mtwara, chama hicho kimerejea kwenye mchakato huo, kubwa linalosubiriwa na wengi likiwa ni vikao vya juu ambavyo ama vitapitisha au kutopitisha majina ya makada wa CCM walioongoza kwenye kura za maoni kusaka kuteuliwa kuwania ubunge.

Wakati wadau wa siasa wakisubiri kufanyika kwa vikao hivyo, chama hicho kimeweka wazi mambo kadhaa ambayo yatasababisha vikao vya juu vya uamuzi kukata jina la mtiania hata kama ameongoza kwenye kura za maoni. Mambo hayo ni pamoja na yanayoendelea kinyume cha katiba, kanuni na maadili ya chama ikiwamo kutoa rushwa, kupendelewa au kubebwa, ubadhirifu wa mali za chama, uzinzi na ulevi.

Mengine yatakayoangaliwa katika vikao hivyo ni pamoja na uzoefu ndani ya chama na namna muhusika anavyojitoa kwa chama bila kusahau mwenendo wake kitabia kama amewahi kuitwa kwenye Kamati za Maadili ya chama.

Katika mazungumzo mahsusi na Nipashe jijini hapa, Katibu wa NEC, Idara ya Organaizesheni ya CCM Taifa, ambaye ndiye msimamizi wa masuala yote ya uchaguzi ndani ya chama hicho, Pereira Ame Silima, alisema vipo vitu vingi ambavyo vinazingatiwa katika kupitisha watiania ikiwa ni pamoja na namna walivyopata kura za maoni.

"Kwanza, kura za maoni amezipataje? Inawezekana amefanya mambo ambayo hayakipendezi chama kama vile rushwa, upendeleo, kampeni zako, umeishije na wenzako, umeishije na chama, umejitoaje kwenye chama.

"Hii ni sehemu kubwa ya mambo kwenye kupata nafasi, inawezekana wewe hautaki kujitoa kwenye chama. Mfano, ukiambiwa hivi, unasema saa hivi sijui hivi, sababu nyingi.

"Pia, unaweza kuwa unafanya kazi na chama lakini ukawa huna maadili, mlevi, mzinzi, mbadhirifu wa mali za chama, na wakati mwingine umeitwa kwenye kamati hizi za maadili, hiyo ni sehemu kubwa sana ya mambo ya kukuondoa, alibainisha.

Silima aliendelea kutaja vigezo vitakavyotumika akisema: "Umeshirikianaje na viongozi wenzako? Je, una heshima na wenzio? Tunaangalia maadili kwa ujumla, huyo aliyeshinda, anaheshimu katiba na kanuni?"

Silima alisema pia wataangalia uzoefu katika kuchambua mtu wa kumteua kupeperusha bendera ya chama chao.

"Maana unaweza kupata kura za maoni lakini hujawahi kukitumikia chama, hujahusika kwenye chama, sasa kupewa nafasi kwenye ubunge ni fursa muhimu ambayo ni vyema huko nyuma ukawa umewahi kufanya shughuli za chama umewahi kuwa hata balozi. Umeanza wapi au wewe ubunge tu ndio kiingilio chako cha mwanzo? Tunazingatia hili," alisema.

Kwa mujibu wa Kanuni za Uteuzi wa Wagombea Uongozi katika Vyombo vya Dola Toleo la Juni 2019, katika uchaguzi na uteuzi wa wagombea, mgombea yeyote wa CCM, anayetaka kuingia katika chombo cha dola, atateuliwa kwa kuzingatiwa kura za maoni zilizopigwa.

Kanuni hizo pia zinabainisha kuwa, mgombea atakayeteuliwa, ni yule anayeongoza kwa wingi wa kura za maoni alizopata, isipokuwa kwamba endapo itathibitika kuwa kura hizo za ushindi alizipata kwa njia ya rushwa, kikao cha uteuzi cha mwisho hakitamteua kugombea nafasi aliyoomba.

Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM (CC), itawajadili wagombea wote na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) kwa ajili ya uteuzi wa mwisho.

CC itakapokuwa inafanya kazi ya kujadili na kutoa mapendekezo, pia itazingatia tathmini itakayokuwa imefanyika ya utendaji kazi wa wabunge na wawakilishi wanaomaliza muda wao.

HABARI KITAIFA

# Serikali yanasa w'biashara sugu utoroshaji madini nje

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imesema inayachunguza majina ya wafanyabiashara wakubwa 12 wa madini, ambao wanadaiwa kuwa ni vinara wa utoroshaji wa vito kwenda nje ya nchi.

Imeelezwa kuwa wafanyabiashara hao hutorosha madini hayo kwa kutumia magodoro, jambo ambalo linakuwa gumu kuwabaini.

Waziri wa Madini, Dotto Biteko, aliyasema hayo wakati akizungumza na wafanyabiashara wa madini jijini Arusha, alipokwenda kushiriki mkutano mkuu wa uchaguzi wa viongozi wa Chama cha Wafanyabiashara, Wauzaji na Wanunuzi wa Madini Tanzania (TAMIDA).

Waziri Biteko alibainisha kuwa tayari majina ya wafanyabiashara hao yametua kwenye mikono yake na kwamba uchunguzi umeshakamilika dhidi yao, kinachofuata ni kuwatia nguvuni.

"Kwa sasa tumeshawachunguza kwa muda wa miezi mitatu tumebaini michezo yao jinsi wanavyotorosha madini kwa kitumia magodoro, sasa kinachofuatia baada ya uchunguzi huu kunyakua mmoja baada ya mwingine," alisema na kuongeza:

"Niseme kweli wapo wafanyabiashara 12 ambao wanatorosha madini, na hao wizara inawajua na itawashughulikia ipasavyo. Na sio hao tu, wapo na wengine wanaoshirikiana nao, hili halikubaliki, hawawezi kukwepa kodi ya serikali ili kujinufaisha wao, kwa kuhujumu nchi," alisema.

Kutokana na tuhuma hizo, aliwaonya baadhi ya wafanyabiashara wa madini ambao wamejenga tabia ya kutorosha madini kwenda nje ya nchi kuacha mara moja ili kuepuka mkono wa dola.

Alisema utoroshaji wa madini ndani ya nchi haulipi, zaidi inalisababishia hasara Taifa, na kuwa ni vema kila mfanyabiashara akafahamu kuwa serikali ina taarifa zote kuhusu utoroshaji wa madini, hivyo ni vizuri watu wakafanya biashara hiyo kwa uaminifu.

"Nashukuru Watanzania ambao ni raia wema wametupatia taarifa za watoroshaji hawa jinsi wanavyotorosha madini yetu," alisema Biteko.

Aidha, Waziri Biteko aliwaomba wafanyabiashara wa madini nchini kuzungumza na wenzao ili waache tabia hiyo inayochafua sekta ya madini. Kuhusu hatua watazochukuliwa, Waziri alisema watatoa taarifa kwenye vyombo vya habari hatua zitakazochukuliwa dhidi yao.

Mbali na hilo, Biteko aliwataka wafanyabiashara wa madini kutunza kumbukumbu za ununuzi na uuzaji wa madini, pamoja na ulipaji mishahara kwa watumishi wao ili waepuke kufanyiwa tathmini kubwa ya ulipaji kodi isiyolingana na kipato chao.

Aliwataka wafanyabiashara kutunza madini yao kwenye soko la madini kama sheria inavyoelekeza na waache kuficha nyumbani.

Kuhusu kero ya biashara ya usonara wa madini ya vito, alisema serikali imeshaunda sheria mpya ya ukataji wa madini ili itumike kuondoa kero hiyo.

"Viongozi watakaochaguliwa naomba wawe wanaifahamu vizuri sekta hii ili wanapokwenda nje ya nchi waisemee vizuri sekta yetu, epukeni kuchagua watu wasioifahamu sekta hii," alisema Biteko.

Aidha, aliwasihi wajumbe wa mkutano huo wa uchaguzi kuchagua viongozi weledi na watakaokuwa kiungo na suluhu kwa changamoto za wachimbaji ili kuleta matokeo chanya.

Mwenyekiti wa TAMIDA aliyemaliza muda wake, Sam Mollel, alisema, Rais John Magufuli ameiwezesha sekta hiyo kukua baada ya kudhibiti utoroshaji wa madini, pamoja na kuifikisha Tanzania katika uchumi wa kati kabla ya mwaka 2025.

## CWT: Tumelipwa malimbikizo bil. 358/- ya likizo, uhamisho

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimesema hadi Juni mwaka huu, serikali imelipa malimbikizo ya madeni ya walimu yasiyo ya mishahara ikiwamo likizo na uhamisho kiasi cha Sh. bilioni 358.1.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa chama hicho, Deus Seif, alipokuwa akizungumza na wanahabari katika kongamano la Mwalimu Baba Lao ambalo liliambatana na kuwaaga walimu wanaotarajia kuhitimu lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Alisema pia kiasi cha Sh. bilioni 38.3 kimelipwa kama malimbikizo ya mishahara kwa walimu 35,805 kwa kipindi hicho.

"Hii inaonyesha nia njema kwa walimu kwa kuwa walichokuwa wanadai kimelipwa, bado serikali itaendelea kulipa madeni haya uhakiki ukikamilika, hivyo tuendelee kuwa na subira," alisema Seif.

Aidha, alisema Juni 5, mwaka huu katika mkutano mkuu wa chama hicho waliomba kupunguziwa uhaba wa walimu, ambapo Rais John Magufuli aliahidi serikali itaajiri walimu 13,000.

Seif alisema hivi sasa walimu wanafanya kazi kwa bidii kutokana na serikali kuwajali na kuwatimizia mahitaji yao kama ilivyo katika sekta nyingine.

"Pia tumeahidiwa walimu 166,548 wanaostahili kupandishwa vyeo wapandishwe ili waweze kupata stahiki zao pale wanapostahili, tunajua wakati wa kupandisha vyeo mwaka 2019/2020 kulikuwa na changamoto ya waraka kuwaacha walimu waliokuwa masomoni, hilo tumeliona na tumewasiliana na mamlaka husika," alisema Seif.

Alibainisha kuwa walimu 106,367 kati ya 267,272 wamepandishwa vyeo na kubadilishiwa mishahara yao ambapo ni sawa na asilimia 40.1.


MCB BANK BETTER TOGETHER
Mwalimu Commercial Bank Plc

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA NNE

1. Taarifa inatolewa kuwa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 4 wa **Mwalimu Commercial Bank Plc** utafanyika katika Ukumbi wa **ISIKE MWANAKIYUNGI – Tabora** Mjini siku ya **Alhamisi, Agosti 13, 2020** kuanzia saa **5:00 Asubuhi**

2. **Ajenda ya Mkutano ni kama ifuatavyo:**
   - 2.1 Kufungua Mkutano
   - 2.2 Kupitishwa kwa Ajenda.
   - 2.3 Uthibitisho wa Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa tatu wa Mwaka 2019
   - 2.4 Kujadili Yatokanayo kwenye Mkutano Mkuu wa tatu wa mwaka 2019.
   - 2.5 Taarifa ya Mwenyekiti
   - 2.6 Kupokea Taarifa ya Wakurugenzi na kupitishwa kwa taarifa za Hesabu za Fedha za Mwaka 2019.
   - 2.7 Gawio
   - 2.8 Kuongeza mtaji wa benki
   - 2.9 Uteuzi wa wakurugenzi huru
   - 2.10 Ada za Wakurugenzi
   - 2.11 Uteuzi wa Wakaguzi wa nje.
   - 2.12 Mapendekezo ya Marekebisho ya MEMARTS.
   - 2.13 Mengineyo yatokanayo na mkutano.
   - 2.14 Tarehe ya mkutano ujao.
   - 2.15 Kufungwa kwa Mkutano.

3. Mwanahisa yeyote ambaye anataka kuingiza pendekezo lake katika kipengele cha 2.13 hapo juu lazima atoe taarifa kwa maandishi siku tatu (3) kabla ya Mkutano Mkuu wa Mwaka.

4. Mwanahisa atakaeshindwa kuhudhuria ana haki ya kuteua mwakilishi kuhudhuria mkutano kwa niaba yake. Taarifa hizi zimfikie Katibu angalau saa arobaini na nane (48) kabla ya wakati wa mkutano.

5. Wanahisa wote wanaombwa kuja na vyeti vya hisa pamoja na vitambulisho siku ya mkutano.

6. Makabrasha ya mkutano yanapatikana kwenye matawi yetu ya Samora Avenue- na Mlimani Dar es Salaam, na katika ofisi zetu za Mwanza, Morogoro na Mbeya pia yatapatikana kwenye ukumbi siku ya mkutano.

7. Gharama za usafiri na malazi zitafanywa na wanahisa wenyewe.

**Mwalimu Commercial Bank Plc**

215839302

**TAARIFA YA SEMINA KWA WANAHISA**

**Taarifa inatolewa kwamba kutakuwa na Semina kwa Wanahisa itakayolenga kutoa elimu kuhusu "Hisa", Elimu ya Fedha na Bidhaa zinazotolewa na Benki ya Mwalimu.Semina hiyo itafanyika Alhamisi,tarehe 13/08/2020 katika Ukumbi wa ISIKE MWANAKIYUNGI Hall -TABORA kuanzia saa 3.00 asubuhi.**

BETTER TOGETHER

Mlimani Tower, Opposite Mlimani City
P.O.Box 61002 , Dar es salaam Tanzania
Tel: +255 22 2775 131



Wawakilishi wa Taasisi ya HAK Humanitarian Aid Organization wakichinja ng'ombe kusherehekea sikukuu ya Idd el Haj kwa ajili ya kuwapa sadaka ya nyama kaya maskini, kambi za wanafunzi na watu wenye uhitaji maalum, mwishoni mwa wiki Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CHADEMA yafafanua ugombea urais Lissu

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetoa ufafanuzi kuhusu Makamu Mwenyekiti, Tundu Lissu, kukabiliwa na kesi mahakamani na iwapo atateuliwa kugombea nafasi ya urais kwa tiketi ya chama hicho, kuwa watazungumza na mawakili wao jinsi ya kumsaidia katika kesi zake ili suala hilo lisiingiliane na ratiba za kampeni.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam baada ya kikao cha Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na vyama vya siasa uchaguzi mkuu, Naibu Katibu Mkuu CHADEMA (Bara), Singo Kigaila, alisema Lissu ni miongoni mwa watia nia saba kiti cha urais kupitia chama hicho.

Lissu alirejea nchini wiki iliyopita akitokea Brussels nchini Ubelgiji, alikokuwa amekwenda kwa matibabu tangu Januari mwaka 2018, baada ya kushambuliwa kwa risasi akiwa nyumbani kwake Dodoma.

Kigaila alisema mchakato wa kumpitisha mgombea kiti cha urais ulianza jana baada ya Kamati Kuu kukaa na leo Baraza Kuu litakutana na Mkutano Mkuu unaotarajiwa kufanyika kesho.

"Kesi haiwezi kumzuia mtu kugombea, kuwa na kesi bado ni mtuhumiwa hajahukumiwa," alifafanua. Alisema kesi haiwezi kumzuia mtu kwende kwenye kampeni za uchaguzi mkuu kwa sababu hazipo kila siku.

"Tunajua zipo kesi zinazomkabili mahakamani na kama ikatokea akateuliwa kuwa mgombea kiti cha urais, mawakili wataona namna gani ifanyike kuhusu hizo kesi. "Kwa vyovyote vile inabidi hakimu au jaji aelewe kuna mtu anagombea urais au ubunge ikiwezekana kesi isimame ili akimaliza kampeni ziendelee."

Kuhusu mkutano huo wa NEC na vyama vya siasa alisema eneo la vipeperushi au mabango ili vitumike ni lazima vipate kwanza idhini kwa Tume au wasimamizi wa uchaguzi ama wasaidizi wa wasimamizi wa uchaguzi lina tatizo.

"Tunaona hili suala ni baya kwa sababu hakuna kanuni, sheria au maelekezo yaliyotolewa kwa watakaofanya maamuzi hayo, watakaoidhinisha watafuata misingi ipi, tunaona hili litaleta shida na Tume itabadilika kuwa tatizo badala ya wawezeshaji," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Anna Henga, akitoa ufafanuzi kuhusu suala hilo, alisema sheria inasema sifa za mgombea asiwe na hatia ya kukwepa kodi.

"Sheria haisemi lolote kuhusu kuahirisha makosa yanayomkabili mgombea. Kwa hiyo kama kuna haja ya kuahirisha utaratibu wa kawaida wa kuahirisha mashauri utatumika," alisema.

Katika kikao hicho cha Tume na vyama vya siasa, Mwenyekiti wa NEC, Jaji wa Rufani mstaafu, Semistocles Kaijage, alisema daftari la wapigakura lina wapigakura milioni 29,188,347.

Alisema bajeti inayotarajiwa kutumika katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28 mwaka huu ni Sh. bilioni 331.7.

Alisema kutakuwa na vituo 80,155 vya kupigia kura na kila kimoja kitakuwa na wapiga kura wasiozidi 500.

Alisema jumla ya asasi za kiraia 97 zenye nia ya kuwa watazamaji wa uchaguzi ndizo zimekidhi vigezo na tayari zimepewa taarifa na zinasubiri kupewa vibali wakati ukifika.

# Agizo la Magufuli barabara kuwekwa mzani latekelezwa

**Na Gwamaka Alipipi**

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), Elias Kwandikwa, ameagiza kuwekwa mzani katika barabara ya Malendegu-Nangurukuru hadi Mbemkulu mkoani Lindi.

Lengo la agizo hilo ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli, la kutaka kuyadhibiti magari yanayobeba makaa ya mawe yasiharibu barabara hiyo.

Vilevile, amesema ukarabati wa barabara hiyo umeshaanza na kwamba unatarajia kukamilika Oktoba, mwaka huu

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya ukarabati wa barabara hiyo, baada ya Rais Magufuli kuagiza kukarabatiwa.

Kwandikwa alisema baada ya kuikagua barabara hiyo walibaini kuwa magari yanayobeba makaa ya mawe kutoka katika mgodi wa Makangaga na kupita katika barabara hiyo ndiyo chanzo cha uharibifu.

"Tulikuwa tunakagua kuona namna nzuri ya kuyasimamia magari yanayobeba mawe na kupeleka viwandani. Tumebaini kuna malori yaliyokuwa yanabeba makaa kuelekea Dar es Salaam yalikuwa yanazidisha uzito na kuharibu barabara, kuna mgodi unaitwa Makangaga ndiko yanakotoka," alisema Kwandikwa.

Kwandikwa alisema kutokana na hali hiyo wameamua kuweka mzani wa kuyapima uzito magari hayo kabla hayajakanyaga barabara hiyo.

Alisema utaratibu utafanyika kwa kusogeza mizani karibu na kiwanda hicho ili kuhakikisha magari yote yatakayopita katika barabara hiyo yawe yanapimwa uzito.

"Tunao mzani wa Nangurukuru ambako ni mbali kutokea hapa, kiasi kwamba hadi gari likapimwe kule tayari uharibifu utakuwa umetokea. Ile sehemu kabla ya kuingia barabara kuu tutaweka mzani. Mwanzo yalikuwa magari machache lakini kwa sasa kutokana na uchumi wa viwanda yamekuwa mengi," alisema Kwandikwa.

Mbali na hilo, Kwandikwa alisema kutatengwa eneo maalum litakalotumika kuyahifadhi mawe hayo kabla ya kuingia katika barabara hiyo.

Alisema Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Eliud Mwakalinga, yupo eneo la tukio tangu Rais Magufuli alipotoa agizo la ukarabati wa barabara hiyo na kwamba maandalizi yanaendelea vizuri.

Aliongeza: "Sina mashaka kwa sababu kubwa lilikuwa ni suala la fedha na hivi sasa Katibu Mkuu wa Ujenzi Mhandisi Mwakalinga ameshalisimamia na mipango inakwenda vizuri."

Aidha, aliwahakikisha wakazi wa mikoa ya Lindi na Mtwara kuwa maeneo ya barabara yaliyokuwa yameharibika yameanza kufanyiwa matengenezo kwa sababu asilimia 80 ya bajeti ya wizara imetengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara nchini.

Katibu Mkuu, Mhandisi Mwakalinga alisema ukarabati wa barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 95 umeshaanza na utakamilika mwezi Oktoba, mwaka huu.

Alisema makandarasi watatu wameshaandaliwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara hiyo ambayo itagawanywa katika vipande vitatu.

Alisema ukaguzi wa barabara hiyo umeshakamilika na muda wowote ukarabati utaanza na kwamba fedha zimeshatengwa.

"Tumeshwasiliana na 'Road Fund' (Mfuko wa Barabara), na wameahidi watatuma fedha katika akaunti ya mkoa muda wowote kuanzia sasa zitaingia ambazo zitatumika kufanya hiyo kazi. Tunataka kipande cha kilometa 95 kukigawa katika vipande vitatu, yaani kila kipande kilometa 30, hivyo tutakuwa na makandarasi watatu. Kipande cha kilometa 60 alichozungumzia Rais kitakuwa na makandarasi wawili," alisema Mhandisi Mwakalinga na kuongeza:

"Sasa makandarasi wote watafanya kazi kwa haraka ili wakamilishe kazi kwa wakati, tunakata ifikapo mwezi Oktoba mradi uwe umekamilika au umefikia hatua za mwisho."

# Bil. 400/- kuokolewa kwa uagizaji nje mafuta ya kula

**Na Ashton Balaigwa,** SIMIYU

TAASISI ya Kilimo Tanzania (TARI) imesema imejipanga kuokoa fedha za serikali zaidi ya Sh. bilioni 400 zinazotumika kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi, kwa kuamua kuongeza uzalishaji wa mazao ya michikichi na alizeti.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI. Dk. Geofrey Mkamilo, alisema hayo wakati Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alipotembea banda la taasisi hiyo katika viwanja vya Nanenane vilivyopo Nyakabindi mkoani Simiyu, ambapo maonyesho hayo yanafanyika kitaifa.

Dk. Mkamilo alisema taasisi hiyo imejipanga kuokoa fedha hizo kwa kuzalisha mbegu bora za michikichi aina ya Tenera pamoja na alizeti ambazo zimeanza kusambazwa kwa wakulima nchini ili kuanza uzalishaji.

Alisema wizara ya kilimo kupitia TARI imedhamiria kutoa mbegu bora za michikichi zitakazotosheleza kupanda hekta 114,000 zilizopo mkoa wa Kigoma zinazofaa kupanda chikichi pamoja na mikoa mingine nchini.

Alisema mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni tani 570,000 katika tani hizo tani 205,000 huzalishwa nchini zilizobaki tani 365,000 ndiyo inayoagizwa kutoka nje.

"Kwenye maduka kuna mafuta yanaitwa Korie yamekuwa yakitumika sana kwa wananchi, lakini hilo ni jina la kibiashara lakini mafuta hayo yanatokana na mawese hivyo tunataka kuzalisha michikichi kwa wingi ili tupate mafuta ya mawese," alisema Dk. Mkamilo.

Alisema wizara pia imepanga mkakati wa zao la alizeti ili kuongeza nguvu ya upatikanaji wa mafuta ya kula nchini kwa sababu ni zao la muda mfupi.

"Kuanzia Januari mwakani tunaweka nguvu zaidi kuhakikisha kazi hiyo inakwenda ya uzalishaji wa mbegu bora za mafuta ziweze kuwafikia wakulima," alisema Dk. Mkamilo.

Alisema kabla ya kuanzishwa kwa TARI Kituo cha Utafiti cha Ilonga kilikuwa kinazalisha wastani wa tani 2.3 za mbegu hizo la alizeti, lakini kwa mwaka wa kwanza baada ya kuundwa kwa taasisi hiyo uzalishaji wa mbegu umeongezeka na kufikia tani 7.5.

# Mil. 57/- zatumika kuokoa watoto njiti

**Na Mwandishi Wetu, BUNDA**

TAASISI ya Vodacom Tanzania, imekabidhi vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 57.8 kwa ajili ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati (Njiti) katika Hospitali ya St. Mary's iliyopo Kibara wilayani Bunda.

Akikabidhi vifaa hivyo mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Rosalynn Mworia, alisema jukumu la taasisi hiyo ni kurudisha tabasamu kwa jamii, hivyo kutoa vifaa tiba kwa ajili ya watoto njiti ni faraja kwa taasisi yake.

"Tunafuraha kuwa sehemu ya kuokoa maisha kwa watoto njiti, maana vifaa tiba hivi vitawasaidia kuendelea kuishi na hivyo kutimiza ndoto na malengo yao hapo baadaye," alisema Mworia.

Alisema kati ya malengo ya Taasisi ya Vodacom Tanzania ni kuokoa maisha ya kinamama na watoto, ndio maana wamekuwa mstari wa mbele katika kuunga juhudi za serikali katika kutokomeza vifo vya mama na watoto nchini.

Mchango wa vifaa tiba ulijumuisha vifaa vya kuokoa maisha kama oksijeni ambavyo vitasaidia watoto njiti kupumua, viongeza joto kwa ajili ya kuhifadhi watoto hao, mashine za tiba mwanga (phototherapy machine) na mashine maalum za kupimia mapigo ya moyo, vitanda vinne, shuka 50 na mablanketi 20.

Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mwanza, Renatusa Nkwande, aliishukuru taasisi hiyo kwa kazi wanayofanya na kwamba wana imani kuwa vifaa vilivyokabidhiwa hospitalini hapo vitatumika kuboresha utoaji na upatikanaji wa huduma bora ya afya kwa watu wengi hususani kinamama na watoto wilayani humo.

# Wakulima waliokopa dawa za mikorosho watakiwa kulipa

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

CHAMA Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wilayani Tunduru mkoani Ruvuma (AMCOS) kimewatahadharisha wakulima wa korosho waliokopa mkopo wa dawa kwa ajili ya kupulizia mikorosho yao, kujiandaa kulipa kwa wakati kwani dawa hizo hazitolewi na serikali kama zawadi.

Hayo yalisemwa na meneja wa chama hicho Imani Kalembo wakati akiongea na viongozi wa vyama vya ushirika vya wakulima AMCOS wilayani Tunduru kwenye kikao kazi cha wadau wa zao la mbaazi kilicho fanyika kwenye ukumbi wa Klasata wa walimu wa Tarafa ya Mlingoti mjini hapa.

Akifafanua taarifa hiyo Kalembo alisema kuwa tahadhari hiyo ameitoa kufuatia kuwapo kwa maombi mengi kutoka kwa wakulima wa zao hilo, huku takwimu za chama hicho zikionyesha kuwapo kwa idadi kubwa ya kiasi kilicho kopwa na wakulima hao.

Alisema hadi sasa chama kikuu kimekwisha pokea tani 900 zenye thamani ya Sh. bilioni 1.191 zimekwisha pokelewa na kusambazwa kwa wakulima na kwamba ili kukidhi maombi ya wakulima hao tayari TAMCU imekwisha agiza tani 100 za dawa hizo na kwamba baada ya kufika yatasambazwa kwa wakulima wenye mahitaji ya kuyatumia katika msimu huu.

Alisema kiasi hicho ni kikubwa mno hata ikilinganishwa na jirani zao wa Wilaya ya Tandahimba ambao mbali na kuwa na uzalishaji mkubwa wa korosho, lakini hadi sasa takwimu zinaonyesha wamekopa tani 600 pekee.

Kufutia hali hiyo Kalembo aliwataka viongozi wa Vyama vya Ushirika Amcos kuweka vizuri kumbukumbu zao za mapokezi ya dawa hizo ili kuondoa utata ambao unaweza kujitokeza wakati wa kukusanya fedha hizo kutoka kwa wakulima kipindi cha ulipaji wake ambapo mkulima aliyekopa mfuko mmoja wa Sulphur atakatwa shilingi 32,000 kwa kila mfuko.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi wa vyama vya msingi wilayani humo, Makamu Mwenyekiti wa TAMCU, Mussa Manjaule alisema ujumbe huo umepokelewa na akaahidi kuwa wataufanyia kazi ili kukiondolea chama kikuu usumbufu ambao kimekuwa kikiupata kutoka serikalini na wadau wengine wa fedha.

Ofisa Tawala wa Wilaya ya Tunduru, Richard Mbambe, aliwataka viongozi wa vyama vya wakulima kuongeza juhudi za utoaji wa elimu kwa wakulima na kufanya vikao vya mara kwa mara ili kuondoa utata ambao unaweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya wakulima.

# Shirika: Suluhisho ukatili wa kijinsia lipo kwa wanaume

**Na Happy Severine,** SIMIYU

SHIRIKA lisilo la kiserikali linalojishughulisha na masuala ya ukatili wa kijinsia Kawie Social Development Foundation (KASODEFO), mjini Maswa, mkoani Simiyu, limesema suluhisho pekee la kukomesha vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto lipo kwa wanaume.

Limesema licha ya serikali na wadau wengine kuendelea kupambana na janga hilo ambalo limeendelea kuwanyima haki za msingi wanawake, litatatuliwa endapo wanaume watashirikishwa katika kupiga vita jambo hilo.

Akiongea na waandishi wa habari kwenye maonyesho ya kilimo na sherehe za wakulima (Nanenane), kitaifa yanayofanyika viwanja vya Nyakabindi mkoa wa Simiyu, Meneja mradi wa shirika hilo, Marius Isavika, alisema wenyewe ndiyo wenye uwezo wa kumaliza tatizo hilo.

Isavika alisema kuwa shirika limeona kuna haja kubwa ya wanaume kushirikishwa kwenye mapambano hayo.

Alisema mradi huo walioanza kutekeleza toka mwaka 2016 chini ya ufadhili wa Shirika la Legal Service Facility (LSF), wamebaini kuwa wanaume hawashirikishwi hali ambayo imesababisha matukio hayo kuendelea kuwapo.

"Mashirika mengi tumeona yamekuwa yakiwashirikisha waathirika pekee (wanawake) katika kupiga vita tatizo hili, lakini ukweli ni kwamba tunakosea, lazima wanaume washirikishwe kila hatua ili waweze kutatua matatizo yao wenyewe," alisema Isavike.

Pia alisema serikali na wadau wengine wabadalishe mfumo kwa sasa na kuanza kuwajumuisha wanaume ili waweze kutambua wanachowafanyia wake zao au watoto wao ni unyama.

Mratibu huyo alisema katika kutekeleza mradi huo, wamegundua kuwa vitendo vimeendelea kuwapo ingawa vinapungua kutokana na wanawake wengi kuanza kutambua haki zao na wapi wapekele matatizo yao. Alisema katika Mkoa wa Simiyu, wanawake wengi hawawezi kumiliki ardhi wala uchumi wa familia, kazi kubwa kwao ni kuzalisha, lakini kwenye haki ya kutumia walichozalisha hawana.

"Wengi hawajui kama ni haki yao kumiliki ardhi, uchumi wa familia, hawajui kama wana haki kwenye mali wanazozalisha, kati ya kesi 10 ambazo tumekuwa tukipokea, nane zinahusu ukatili wa kijinsia na migogoro ya ardhi," alisema Isavike.

Mratibu huyo alisema shirika hilo limeshiriki maonyesho hayo kwa lengo la kutoa elimu kwa jamii jinsi ya kupambana na ukatili ikiwa pamoja na kutoa msaada wa kisheria kwa wenye matatizo.

Aliwataka wananchi wote wa mkoa wa Simiyu na mikoa jirani kufika kwenye banda hilo kwa ajili ya kupata elimu ikiwa pamoja na kupewa msaada wa kisheria kwa wenye matatizo mbalimbali yanayohitaji msaada wa sheria.

**"Mashirika mengi tumeona yamekuwa yakiwashirikisha waathirika pekee (wanawake) katika kupiga vita tatizo hili, lakini ukweli ni kwamba tunakosea, lazima wanaume washirikishwe kila hatua ili waweze kutatua matatizo yao wenyewe,"**


## TUMAINI UNIVERSITY MAKUMIRA

**P. O. Box 55, USA-RIVER, ARUSHA**
**Tanzania, East Africa**

## JOB VACANCIES

Tumaini University Makumira (TUMA) invites qualified applicants from recognized institutions of higher learning to be considered for employment in the following teaching posts:

1. **Lecturers or Assistant Lecturers in Physics**
2. **Lecturers or Assistant Lecturers in Chemistry**
3. **Lecturers or Assistant Lecturers in Mathematics**
4. **Lecturers or Assistant Lecturers in Biology**

Qualifications:

- A minimum GPA of 4.0 in Master of Science or Master of Science with Education in the specified teaching subjects.
- A minimum GPA of 3.5 in Bachelor of Science or Bachelor of Science with Education in the specified teaching subjects
- PhD in Science or Science with Education with a minimum GPA of 4.0 in Master of Science in the specified subjects and a minimum GPA of 3.5 Bachelor of Science or Bachelor of Science with Education in specified subjects.

**Duties:**

- To teach Physics, Chemistry, Mathematics, Biology and educational subjects in the undergraduate programmes.
- To participate in the in-service training activities of Participatory and Integrative Teaching Approach Project, an outreach project of Tumaini University Makumira in 24 secondary schools of Arumeru District.
- To conduct research in your related disciplines.
- To attend academic meetings and perform any other academic duty when assigned by relevant authorities at TUMA

Application letters with the attached CVs, copies of certificates and transcripts have to be sent before **Monday, 16th August 2020** to:

**THE VICE CHANCELLOR,**
**TUMAINI UNIVERSITY MAKUMIRA,**
**P. O. Box 55, USA-RIVER, ARUSHA.**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Usajili Simba, Namungo umulike michuano CAF

**DIRISHA** la usajili Ligi Kuu Bara limefunguliwa tangu mapema Jumamosi Agosti Mosi, mwaka huu na linatarajiwa kufungwa rasmi mwishoni mwa mwezi huu, na tayari baadhi ya klabu zimeshaanza kujiimarisha kwa ajili ya msimu ujao.

Hata hivyo, baada ya mtifuano mkali msimu huu ambao umeshuhudiwa timu tano za Ligi Kuu Bara zikishuka daraja; Singida United, Alliance, Ndanda, Lipuli FC na Mbao FC, msimu ujao pia unatarajiwa kuwa ngumu zaidi kutokana na kushirikisha jumla ya timu 18 tu badala ya 20 za msimu uliomalizika.

Hivyo, klabu zinapaswa kufanya usajili makini zaidi na kujitahidi kuwa na vikosi vipana ili kuweza kuhimili mikikimiki ya ligi hiyo inayotarajiwa kuanza katikati mwa mwezi ujao.

Aidha, klabu za Simba na Namungo FC mbali na michuano ya ndani Ligi Kuu Bara na Kombe la Shirikisho Soka nchini (FA Cup), zinapaswa kuwa makini zaidi katika dirisha hili la usajili kutokana na jukumu kubwa lililo mbele yao la kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu.

Simba ambayo imetwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu, ikiwa ni mara ya tatu kwao mfululizo, itapeperusha bendera ya nchi kwenye kinyang'anyiro cha Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Namungo FC ikibeba jukumu la kuhakikisha bendera hiyo inapepea vema katika Kombe la Shirikisho Afrika.

Namungo ambayo ilicheza mechi ya fainali ya Kombe la FA jana dhidi ya Simba katika Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga, hata kabla ya matokeo ya jana, tayari ilishapata tiketi hiyo ya kushiriki michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kutokana na wapinzani wao, Simba kuwa na tiketi ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara. Hivyo, kutokana na majukumu hayo ya ndani na kuiwakilisha nchi kimataifa, ni wazi Simba na Namungo zinapaswa kuwa na vikosi vipana zaidi vyenye wachezaji wazoefu wa mechi za kimataifa ili kufanya vizuri. Tunasema hivyo kutokana na ukweli kwamba bila kuwa na vikosi vipana vitakavyoziwezesha kuwachezesha kwa mzunguko lakini usajili ukimulika ubora na uzoefu, ni wazi wachezaji watachoka kutokana na kukabiliwa na mechi nyingi.


Imekuwa kawaida kusikia timu za Tanzania zikidai kufanya vibaya kwenye michuano hiyo kumetokana na ratiba ngumu za ligi zinazochangia wachezaji wao kuchoka, huku suala la kutokuwa na nyota wazoefu likichukua nafasi kubwa zaidi, hivyo kipindi hiki hatutarajii kusikia kauli kama hizo kwa kuwa muda wa kujipanga upo na TFF kwa kipindi cha misimu miwili iliyopita, imekuwa ikizingatia ratiba rafiki kwa wawakilishi wetu.

Kwa upande wa Simba, kama ni michuano ya ndani, Nipashe tunakiri imekamilika kila idara na inaweza kuwaandaa wachezaji walio nao kikosini na kuweza kutetea ubingwa, lakini linapokuja suala la mechi za kimataifa, kuna idara nyingi inapaswa kusajili nyota bora zaidi na wazoefu.

Huku kwa Namungo ambayo imemaliza Ligi Kuu ikiwa nafasi ya nne nyuma ya Simba, Yanga na Azam FC, ikipaswa kujiimarisha zaidi kwa kumulika wachezaji wazoefu wa michuano ya kimataifa na watakaoweza kwenda kutoa ushindani na si kuishia tu kuweka rekodi ya kushiriki kwa mara ya kwanza michuano hiyo ya pili kwa utajiri barani Afrika kwa ngazi ya klabu baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa.

Kwa hilo, tunaamini huu ni wakati sasa kwa wawakilishi wetu hao kwenye michuano ya kimataifa, kujipanga kufanya usajili makini utakaozifanya kupeperusha vema bendera ya nchi na hata kutwaa ubingwa. Tunatarajia kuona Simba na Namungo zikiwa na mtazamo mpana zaidi katika usajili wao kwa kumulika nyota wazoefu hususan wale wanaopata nafasi katika timu zao za Taifa ambao wanautajiri mkubwa wa uzoefu wa michuano hiyo. Matarajio yetu ni kuona Simba na Namungo zinavunja mwiko kwa kutwaa mataji hayo makubwa kwa klabu barani Afrika na hilo linawezekana kwa kuwa makini katika dirisha hili la usajili ikiwa ni pamoja na kuimarisha vema mabenchi yao ya ufundi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Mbao ilivyosahau kuwa biashara huwa ni asubuhi

**KIPENGA** cha mwisho kilipopulizwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Jumamosi iliyopita, wachezaji wote wa Mbao FC walianguka chini, wengine wakiangua kilio kwa uchungu.

Ni baada ya dakika 90 za machozi jasho na damu, ilipocheza dhidi ya Ihefu FC kutoka Mbarali mkoani Mbeya. Pamoja na ushindi mnono wa mabao 4-2, Mbao FC ilijikuta ikishuka daraja. Hii imetokana na mechi ya kwanza iliyocheza ugenini kukubali kipigo cha mabao 2-0. Ukichanganya na matokeo hayo ni kwamba Mbao na Ihefu zilikuwa zimefungana 4-4, hivyo Ihefu imetinga Ligi Kuu kwa kanuni ya bao la ugenini.

Ilikuwa ni mechi kali ya mchujo kutafuta timu itayokwenda Ligi Kuu, kati ya timu ya Ligi Kuu Mbao FC na timu ya Daraja la Kwanza, Ihefu FC.

Hakika ilikuwa ni siku mbaya si kwa wachezaji na viongozi wa Mbao FC tu, bali ni kwa mashabiki wa soka wa Mwanza, ambao siku si nyingi zilizopita waliipoteza timu ya Alliance FC ambayo yenyewe ilishuka moja kwa moja licha ya kuichapa Namungo FC mabao 3-2 kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

Ilikuwa ni kama marudio tu, kwani Mbao nayo ikiwa nyumbani, licha ya ushindi wa mabao 4-2 nayo ikashuka. Kwanza nikayakumbuka maneno ya straika hatari wa Mbao FC, Waziri Junior, ambaye kwenye Ligi Kuu alifunga mabao 13 na katika mechi hiyo ikifunga mawili.

Baada ya mechi ya kwanza huko Mbarali, aliwaonya Ihefu FC kuwa wasitarajie kuwa watapata mteremko au itakuwa rahisi kwao kupanda Ligi Kuu, kwani watakutana na wakati mgumu wakiwa CCM Kirumba na itakuwa ni mechi ngumu kwao kuliko yeyote ile waliowahi kucheza msimu huu.

"Tunakubali tumefungwa, lakini ukiangalia uwanja haukuwa rafiki kwetu, una mabonde mengi tu, kwa hiyo ilikuwa inatupa tabu sana, lakini nawaambia Ihefu hivi, wao wameshinda kwao na sisi tunawakaribisha kwetu CCM Kirumba, haitokuwa mechi rahisi kwao," alisema Waziri.

Na kweli ilikuwa hivyo. Waziri Junior mwenyewe aliwapa tabu sana mabeki wa Ihefu na kufunga mabao mawili. Lakini wachezaji wa Mbao FC walikuwa wakicheza kana kwamba ni fainali ya Kombe la Dunia. Ikanishangaza sana, ni kwa nini Mbao FC kwa sasa imekuwa ikicheza vizuri na wachezaji wake kujituma kwenye mechi za mwisho, hasa hizi za kuamua matokeo.

Nikajiuliza hivi kweli Mbao FC ingeanza kucheza hivi tangu Ligi Kuu Tanzania Bara inaanza, si ingekuwa inawania nafasi ya pili au ya tatu?

Nikamkumbuka Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda ambaye katika tathmini yake baada ya Ligi Kuu kumalizika, aliziambia timu zingine za ligi kuwa zisizubiri hadi kwenye mechi za mwisho za ligi ili zikaze msuli, badala yake zianze tangu mwanzo kama wao, Coastal Union walivyofanya, ndiyo maana hata mechi za mwisho pamoja na kutofanya vizuri sana, lakini ilikuwa salama.

"Tumejifunza kuwa tukianza kushindana basi anza mwanzo, usisubiri mwisho. Unaona sisi tulianza kupambana mwanzo hatukupata matatizo mwishoni mwa ligi, lakini angalia timu zilizokuwa zikiona kama ligi bado, zilivyopata shida mwishoni," alisema Mgunda.

Hiki ndicho kilichoikuta Alliance FC, Ndanda FC na Lipuli, lakini mwisho wake ikaja kuikuta Mbao FC.

Mfano Mbao FC ilicheza mechi saba za Ligi Kuu, ikashinda sita na kutoka sare moja, ilichowasaidia ni kutoshuka moja kwa moja tu, badala yake ikawa kucheza mechi ya mchujo.

Unajiuliza kama Mbao FC ingeshinda mechi hizo mwanzoni mwa ligi, halafu wachezaji wa timu hiyo wangekuwa wanacheza kwa kujituma kama hizi mechi za hivi karibuni, sidhani kama ingefikiriwa hata kucheza mechi ya mchujo, achilia mbali kushuka.

Kilichotokea CCM Kirumba ni somo kwa timu zingine zilizopo Ligi Kuu na zilizopanda kupambana kuanzia mwanzo hadi mwishoni mwa ligi na si kusubiri mechi za mwisho. Waswahili wanasema biashara asubuhi, jioni mahesabu. Lakini Mbao kwao jioni ndiyo walikuwa wanaanza biashara.

# Samia apigia debe mikopo wakulima, wavuvi, wafugaji

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu, ametoa wito kwa taasisi za kifedha nchini kuongeza kasi ya utoaji wa mikopo kwa wakulima, wavuvi na wafugaji ili waweze kuongeza mitaji na uzalishaji ili waongeze tija zaidi katika ukuaji wa uchumi wa taifa.

Makamu wa Rais alitoa wito huo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizindua Maonyesho ya Kilimo ya Nanenane 2020 yanayofanyika kitaifa kwenye Uwanja wa Nyakabindi, Bariadi mkoani Simiyu yakiwa na kauli mbiu ya "Kwa Maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Chagua Viongozi Bora 2020".

Alisema licha ya taasisi hizo kuwa wachangiaji wakuu wa maendeleo ya sekta za kilimo, mifugo na uvuvi, bado kuna umuhimu kwao kuongeza kasi ya utoaji wa mikopo kwa wadau wa kilimo huku akibainisha kuwa kwa kipindi hiki ni asilimia tisa (9) tu ya mikopo iliyotolewa na taasisi hizo ndio imekwenda kwenye sekta ya kilimo.

Kwa upande wake, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema kuwa wizara yake imeanzisha mpango mpya wa usajili wa wakulima ili kuiwezesha serikali kujua taarifa zote muhimu kuhusu wakulima ikiwamo aina ya mazao wanayozalisha, kiwango cha uzalishaji wao na aina ya msaada wanaohitaji kutoka kwa serikali. Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema taasisi za fedha ikiwamo benki hiyo zina nafasi kubwa kuboresha ustawi wa sekta ya kilimo nchini na ndio sababu benki hiyo imekuwa ikibuni huduma mbalimbali zinazolenga kuwasaidia wadau wa sekta hiyo muhimu, huku akitolea mfano huduma mpya inayotolewa na benki hiyo ikifahamika kama 'NBC Shambani'.

"Tunajivunia kuwa sehemu ya maonyesho haya tukiwa kama washiriki na wadhamini muhimu. Maendeleo ya kilimo nchini yamekuwa ni miongoni mwa vipaumbele vyetu na tunakuwa mstari wa mbele kukuza sekta hii muhimu," alisema Sabi.

Alisema benki hiyo imekuwa ikidhamini maonyesho hayo kwa mwaka wa tatu mfululizo ambapo kwa mwaka huu imechangia udhamini wa kiasi cha Sh. milioni 40 ili kufanikisha maonyesho hayo.

Zaidi Sabi alibainisha kuwa benki hiyo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), wameandaa mafunzo maalumu kwa wafanyabiashara wakiwamo wadau wa kilimo katika kipindi chote cha maonesho hayo wakilenga kuwajengea uwezo zaidi kibiashara wadau hao.

Maonyesho hayo yanalenga kutoa jukwaa kwa wadau wa kilimo nchini kubadilishana utaalamu hususani kiteknolojia, kutafuta masoko mapya sambamba na kupata fursa ya kukutana na watunga sera muhimu kuhusu sekta hiyo.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu (kushoto), akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, machapisho maalum kuhusu mwongozo wa kitaifa kuhusu lishe wakati wa uzinduzi wa maonyesho ya 27 ya kilimo na mifugo (Nanenane) kwenye viwanja vya Nyakabindi, Bariadi mkoani Simiyu. Benki hiyo ni moja ya wadhamini wa maonyesho hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajawazito waonywa matumizi dawa mitishamba

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAJAWAZITO wilayani Kahama wameshauriwa kuacha kutumia dawa za miti shamba kwa ajili ya kuongeza uchungu kwa kuwa dawa hizo ni kali na hupasua mfuko wa uzazi na kusababisha mtoto tumboni kunywa maji machafu.

Ushauri huo ulitolewa na Ofisa Muuguzi wa Halmashauri ya mji wa Kahama, David Luhaga, wakati akizungumza na vyombo vya habari, kuwa wajawazito wengi hasa walioko vijijini wanatumia dawa za kienyeji bila kujua athari zake huku wengine wakishinikizwa na ndugu au jamaa.

Alisema wajawazito wengi hasa wanaoishi pembezoni mwa mji wanatumia dawa za mitishamba kutibu ugonjwa wa minyoo au kuongeza uchungu wakati muda wa kujifungua unapokaribia na kusababisha kupoteza mama na mtoto kwa pamoja na zaidi kutokwa na damu nyingi wakati wa kujifungua.

"Mjawazito anapotumia dawa za kuchochea uchungu na kujifungua mapema inasababisha kuleta madhara makubwa kwa mjamzito ikiwamo kupoteza maisha, aidha kwa mama au mtoto, lakini pia wakati mwingine wanajifungua mtoto akiwa ameshakufa," alisema Luhaga.

Msimamizi wa wodi ya wazazi, Partricia Samson, alisema wanakosa ushirikiano kutoka kwa mjamzito kwa kuwa anakua na maumivu makali na msaada pekee alionao kwa wakati huo ni mkunga aliye karibu naye.

Aliwasihi wajawazito wanapoona dalili za hatari kama kichwa kuuma wafike hospitali au vituo vya afya vilivyopo karibu mapema ili wapate huduma kwa uhakika na usalama zaidi.

# Serikali yafutia mkataba makandarasi mradi maji

**Neema Emmanuel,** GEITA

MAKANDARASI wa Kampuni ya PET Corporation Ltd na Albalwani Investment wamefutiwa mkataba baada ya kushindwa kutekeleza kwa wakati mradi wa maji wa Nyamtukuza uliopo Wilaya ya Nyang'wale, mkoani Geita.

Akizungumza wakati akikagua mradi huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Anthony Sanga, alisema mradi huo unaogharimu Sh. bilioni 15.81 ulianza kujengwa tangu mwaka 2014 na ulitarajiwa kuhudumia wakazi 38,000.

"Mradi ulitakiwa kukamilika ndani ya miezi sita, lakini mpaka 2020, takribani miaka sita utekelezaji wake ni asilimia 65, hivyo serikali imeamua kuvunja mkataba na kazi hiyo sasa itafanywa na wataalamu wa ndani wa mamlaka za maji za mikoa ya Mwanza, Geita na Shinyanga," alisema.

Alisema kusuasua kwa mradi huo kumesababisha wananchi wa maeneo hayo kuendelea kukosa majisafi na salama na kuhatarisha afya zao.

Sanga alisema, hawawezi kuendelea kufanya kazi na wakandarasi hao na kuonya makandarasi wengine ambao kazi zao zinasuasua watapokonywa na kupewa wataalamu wa ndani.

Aliwataka watendaji wote wa maji Mkoa wa Mwanza, Shinyanga na Geita, kuungana na kuweka kambi wilayani humo eneo la mradi na kujenga ndani ya siku 60.

"Haiwezekani tukaendelea kuwabembeleza wakandarasi, miradi yote ya maji ambayo inasuasua sisi tunakwenda katika maeneo hayo tunawapokonya na tunawapa wajenge wataalamu wetu wa ndani ndio maana leo tumesitisha mkataba wa wakandarasi na maelekezo yetu ni kwamba hizi siku mbili, tatu zinatosha wataalamu wetu wa ndani kumaliza kuhamasishana (kujimobilizer) na Jumatano waripoti kwa Mkuu wa Wilaya, ndani ya siku 60 mradi uwe umeanza kutoa maji," alisema.

Mkurugenzi wa Ufundi wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA), Deusdedith Magoma, alisema wamepokea maelekezo kutoka kwa Katibu Mkuu na watatekeleza maelekezo hayo na kusimamia mradi huo usiku na mchana ili uweze kukamilika kwa kipindi hicho.

"Ni muahidi kwamba tutaweza kutekeleza mradi huo chini ya siku 60 kama alivyotuelekeza, sisi tupo tayari Jumatano ya Agosti 5, kuanza kazi," alisema.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Geita, Nicas Ligombi, alisema kwa sasa wanasimamia na kujenga na utakapo kamilika mradi huo kwa kuanzia utanufaisha vijiji 12 vya wilaya hiyo na wananchi 38,000 na baadaye utaruhusu kupanuliwa na kunufaisha watu 140,000.

Charles Masatu mkazi wa Mtukuza na Masurwa Iddi, mkazi wa Mtakuja, walisema wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya ukosefu wa majisafi kwa muda mrefu baada ya mradi huo kusuasua, lakini agizo la kiongozi huyo limerudisha matumaini.

"Kukosekana kwa majisafi na salama kunatalazimu kutumia maji yasiyo safi hivyo mara kwa mara tunakabiliwa na magojwa mbalimbali," alisema Masatu.

# JPM apokea hati za mabalozi wa Marekani, Vietnam

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS John Magufuli jana alipokea hati ya utambulisho za mabalozi wateule wa Marekani na Vietnam nchini.

Balozi wa Marekani hapa nchini ni Dk. Donald Wright na Balozi wa Vietnam ni Nguyen Doanh.

Hafla ya kupokea hati hizo ilifanyika jana Ikulu jijin Dar es Salaam na kurushwa moja kwa moja kupitia vyombo vya habari.

Akizungumza baada ya mabalozi hao kukabidhiwa hati hizo, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema Tanzania imekuwa na uhusiano mzuri na nchi hizo.

Prof. Kabudi alisema ni mwaka wa 55 tangu Tanzania na Vietnam kuanzisha uhusiano wa kibalozi tangu mwaka 1965, na kwamba mahusiano miongoni mwa nchi hizo yamekuwa mazuri hususani katika uwekezaji wa kampuni ya simu ya Halotel.

Kwa upande wa Marekani, Prof. Kabudi alisema tukio hilo ni kubwa sana na ni muhimu kwa sababu linadhihirisha uhusiano mzuri uliopo kati ya Marekani na Tanzania.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitano, Marekani haikuwa na Balozi anayewakilisha nchi hiyo nchini.

"Ni miaka mitano tangu balozi wa mwisho wa Marekani hapa Tanzania kuondoka, haikuwa imeteua Balozi tangu kipindi hicho. Nishukuru Rais John Magufuli kwa uamuzi aliouchukua wa kumwandikia barua Rais wa Marekani, Donald Trump, kumweleza kwamba uhusiano wa Tanzania na nchi hiyo ni mzuri na ni wa muda mrefu," alisema Prof. Kabudi.

"Na Balozi huyo wa Marekani amefurahi kuja Tanzania na ameelezea mahusiano makubwa na mazuri yaliyopo kati ya nchi hizo."

Prof. Kabudi alisema uhusiano wa Tanzania na Marekani ni mzuri sana, na kwamba nchi hiyo imekuwa ikiwekeza katika sekta mbalimbali nchini ikiwamo afya, maji, kilimo, biashara na elimu na hata kuongeza ajira.

## Vyama vyatakiwa kufanya kampeni kistaarabu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VYAMA vya siasa vimetakiwa kufanya kampeni za kistaarabu katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Shekhe wa Wilaya ya Kondoa, Mustaph Mbuva, alipokuwa akizungumza na waumini kwenye Baraza la Eid El Hajj lililofanyika Kingale wilayani Kondoa.

Alisema vyama hivyo vinapaswa kuhakikisha kampeni hazileti mgawanyiko ili kuwapata viongozi watakaolitumikia taifa.

Mbuva alisema kuwa Watanzania ni tarajio lao kubwa kuwapata viongozi wenye kuleta maendeleo na watakaodumisha amani na si vinginevyo.

"Wanasiasa na wagombea watakaopitishwa na vyama vyao vya siasa wafanye kampeni ambazo zitakuwa za ustaarabu na kuepukana na vurugu," alisema.

Aliwataka waumini wa dini hiyo wa Wilaya ya Kondoa kuendelea kuomba kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika ili kuendelea kuwa na amani na kupata viongozi bora.

"Suala la kumtanguliza Mungu kwenye uchaguzi huu, ni muhimu kama tunavyosisitizwa na Rais wetu ambaye amekuwa akifanya hivyo na tunaona mafanikio yake," alisema.

Aliwaomba Watanzania kutofanya makosa kwenye uchaguzi huo kwa kuchagua viongozi ambao watakwamisha maendeleo yao.

"Uchaguzi huu mchague viongozi watakaokuwa na moyo wa utumishi kama ilivyo kwa kiongozi wetu ambaye ni Rais John Magufuli anayetuongoza kwa vitendo," alisema.



Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu (kushoto), akikagua maendeleo ya ujenzi wa majengo katika makao ya Taifa ya Watoto Kikombo mkoani Dodoma, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mchakato sensa ya kilimo, mifugo waanza

**Na Ashton Balaigwa,** SIMIYU

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS) leo inatarajia kuanza rasmi mchakato wa kufanya sensa ya kilimo na mifugo nchini, lengo kuu likiwa ni kupata takwimu halisi.

Akizungumza na Nipashe katika viwanja vya maonyesho ya wakulima na wafugaji vya Nyakabindi vilivyopo mkoani Simiyu, Mtakwimu Mwandamizi kutoka NBS, Samuel Kawa, alisema madhumuni ya sensa hiyo ni kupata taarifa muhimu za kilimo, mifugo na uvuvi zitakazotumika katika kupanga kutathmini utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo.

Alisema sensa hiyo ambayo hufanyika kila baada ya miaka kumi, baadhi ya taarifa ambazo zitakusanywa ni pamoja na kiasi cha uzalishaji wa mazao, idadi ya mifugo na mazao yake, ufugaji wa samaki, usindikaji wa mazao na uhifadhi wa mazao.

Taarifa nyingine zitakazokusanywa ni pamoja na uwekezaji katika kilimo, upatikanaji na matumizi ya mikopo kwa shughuli za kilimo pamoja na huduma za ushauri wa kilimo.

Mtakwimu huyo Mwandamizi, alisema kuwa takwimu hizo zitakusanywa kwa njia ya sampuli kwa wakulima wadogo lakini kwa wakulima wakubwa watahojiwa pamoja na taarifa zinazohusu upatikanaji wa huduma za jamii zitakazotolewa na viongozi wa vijiji.

Akifafanua kuhusu sensa hiyo kisekta kwa upande wa kilimo, alisema kilimo cha mazao taarifa muhimu zitakazokusanywa zitajumuisha ushiriki wa kaya katika shughuli mbalimbali za uzalishaji wa mazao, matumizi ya pembejeo, usindikaji, huduma za ugani pamoja na vikwazo katika kilimo.

Kwa upande wa mifugo, alisema taarifa muhimu zitakazokusanywa ni pamoja na idadi ya mifugo, mazao ya mifugo, magonjwa ya mifugo, masoko na upatikanaji wa huduma za mifugo.

Alisema kwa upande wa ufugaji wa samaki taarifa zitakazokusanywa ni pamoja na aina ya samaki wanaofugwa, miundombinu ya ufugaji, taarifa za uvunaji na masoko.

Naye Ofisa Habari wa NBS, Emmanuel Ghula, alisema takwimu zitakazozalishwa kutokana na sensa hiyo zitasaidia serikali kuainisha maeneo yanayokabiliwa na visumbufu au magonjwa ili kuchukua hatua stahiki za kupanga mipango ya kudhibiti.

Alisema taarifa kuhusu upatikanaji wa ardhi zitatumika katika kupanga mipango ya matumizi bora ya ardhi vijijini ili kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji.

Sensa ya kilimo, mifugo na uvuvi mara ya mwisho ilifanyika mwaka 2007/2008 na hii ni sensa ya tano tangu Tanzania ipate Uhuru.

## TASAF yataka usimamizi mzuri uhakiki kaya maskini

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

WENYEVITI wa Serikali za Mtaa Manispaa ya Morogoro wametakiwa kusimamia vizuri uhakiki wa majina ya walengwa wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kabla ya malipo awamu ya pili hayajafanyika.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani wa mfuko huo, Christophar Sanga na kuwataka wanaohakiki majina ya walengwa wakiwamo wenyeviti wa serikali za mitaa kufanya kazi kwa uhakika.

"Napenda kutoa rai yangu kwa wahusika wote wanaohakiki majina ya walengwa wa mfuko huu wa kuokoa kaya maskini kufanya kazi kwa weledi ili fedha zote zitakazotolewa ziwafikie walengwa wenye sifa na vigezo," alisema Sanga.

Aliwataka waratibu wa mradi huo ngazi za mitaa kuhakikisha wanaweka watu wenye sifa ili kuondoa sintofahamu kwenye baadhi ya maeneo ambayo yameonekana kuwapo kwa watu wasiostahili.

Sanga alisema katika awamu ya pili ya ugawaji wa fedha kwa ajili ya kusaidia kaya maskini nchini ofisi yake haitegemei kuona wala kusikia malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa kuna baadhi ya walengwa wasio na sifa.

Alisema kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wakidai kutotendewa haki kwa kunyimwa fursa ya kuingizwa kwenye mpango huo licha ya kuwa na sifa na wahusika wanatakiwa kubadilika ili kuondoa malalamiko hayo nchini.

Alisema uhakiki utakapokamilika malipo yote yataanza kufanyika mwezi ujao na kuwataka walengwa wote kuzitumia vizuri fedha watakazozipata kufanya shughuli za ujasiriamali ili ziwanufaishe.

Mjumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mfuko wa TASAF nchini, Rogatus Mativila, aliwataka watu wote watakaopata fursa ya kuwa kwenye mpango huo wa kuokoa kaya maskini kuepuka matumizi ya pombe.

# TALGWU yalalamika watumishi kushikiliwa bila kupelekwa kortini

**Restuta Damian,** BUKOBA

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) Mkoa wa Kagera, kimeomba kuwafikisha mahakamani wafanyakazi 34 wa Serikali za Mitaa Halmashauri ya Wilaya Biharamulo wanaotuhumiwa kwa kosa la upotevu wa fedha za makusanyo ya mapato.

Watuhumiwa hao ambao walifikishwa katika kituo cha Polisi Biharamulo na Lusahunga kwa tuhuma za upotevu wa kiasi cha zaidi ya shilingi milioni 307 fedha ambazo hazikuonekana katika mfumo wa mapato ya halmashauri hiyo.

Mwenyekiti wa chama hicho, Mkoa wa Kagera, Naseeb Maselle, alisema wafanyakazi wanaotuhumiwa ni watendaji wa vijiji na kata pamoja na wahasibu na watumishi wa vituo mbalimbali vya afya tuhuma zilitolewa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Marco Gaguti, Juni 23, mwaka huu. Alisema hivi karibuni kamati tendaji ya chama cha wafanyakazi ilikaa na kubaini kuwa watumishi hao hawajawahi kupelekwa mahakamani bali wapo katika vituo vya polisi, jambo ambalo linaendelea kuibua maswali mengi.

Aidha, alisema kamati ya chama cha wafanyakazi ilipata muda wa kujadili malalamiko ya mashine za kukusanya mapato kwa njia ya kielektroniki (EFD) ambazo zimekuwa zikitumiwa na watendaji hao kuwa zimekuwa zikionyesha changamoto mbalimbali.

"Tunashuhudia mashine wanazotumia polisi, watu wa misitu na mamlaka nyingine kuwa anayetoa lisiti kwa mteja naye anabaki na lisiti, lakini zinazotumiwa na watendaji wetu hazina lisiti inayobaki kwa mkusanyaji," alisema na kuongeza: Haya ni mapungufu makubwa, lakini wanaokusanya mapato ya halmashauri hawana elimu ya kutosha juu ya kukusanya mapato."

Hata hivyo, alisema baada ya wafanyakazi hao kukamatwa Juni 23 mwaka huu, Juni 26, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Wende Ng'hala, aliandika barua kwa ofisa wa TAKUKURU wilaya hiyo yenye kumbukumbu namba BDC/12/34/vol/11/08 kuwa baadhi ya watumishi walioshtakiwa hawajawahi kudaiwa na halmashauri na hawahusiki kabisa na upotevu wa fedha, hivyo waachiliwe huru.

Aliongeza kuwa wafanyakazi hao wamekaa zaidi ya mwezi mmoja baada ya kushikiliwa tangu Juni 23 na hakuna taratibu zinazoendelea ili kujua hatima ya wafanyakazi hao.



Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) tawi la Mkoa wa Mtwara, Farida Selemani, akizungumza kwa lugha ya alama na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi wa majimbo 10 ya mkoa huo (hawapo pichani) kwenye mafunzo ya kuimarisha ushiriki wa wenye ulemavu wa kusikia katika uchaguzi mkuu mwaka huu, yaliyofanyika jana mjini Mtwara. **PICHA: HAMISI NASRI**

# TBS yawapa vyeti, leseni wazalishaji

**Na Joseph Mwendapole**

WAZALISHAJI 141 wakubwa, wakati na wadogo nchini wamekabidhiwa vyeti na leseni za kutumia alama ya ubora ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), baada ya bidhaa wanazozalisha kuthibitishwa kukidhi viwango vya ubora.

Kati ya wazalishaji hao 58 ni wazalishaji wadogo ambao wanazalisha bidhaa mbalimbali ikiwamo vitakasa mikono, vyakula, vilainishi, vifaa vya umeme na vya ujenzi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya kukabidhi leseni hizo kwa wazalishaji hao, Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngeya, alisema imekuwa ni kawaida shirika kuwakabidhi vyeti na leseni za kutumia alama ya ubora wazalishaji ambao wanakidhi vigezo ili waendelee na uzalishaji wa bidhaa zenye ubora.

Alisema hatua ya bidhaa hizo kupatiwa vyeti na leseni ya kutumia alama ya ubora ya shirika hilo kutawafanya wazalishaji hao kuwa na uwezo wa kushindana na bidhaa nyingine sokoni, kuuza nchi za Afrika Mashariki bila bidhaa zao kulazimika kupimwa tena kwa ajili ya kuzithibitisha ubora na watapanua wigo wa biashara zao kwa kuyafikia masoko mengi zaidi.

"Ni wakati mwafaka wa kuwapongeza na kuwapa moyo wajasiriamali wadogo ili nao waweze kuwa wakubwa kama wengine, tunakabidhi vyeti na leseni za ubora kwa wajasiriamali na kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu na hii ni kawaida yetu kila baada ya miezi mitatu kuwapongeza baada ya kupata vyeti vyao vya ubora na leseni," alisema na Dk. Ngenya na kuongeza:

"Namshukuru Rais John Magufuli kwa kutoa fursa kwa ajili ya kuhudumia wajasiriamali wadogo bure pale wanapoomba bidhaa wanazozalisha wenyewe kuthibitishwe ubora na TBS."

Aliwataka wajasiriamali hao kuwa mabalozi wazuri wa TBS kwa kuhamasisha wananchi wanaojihusisha na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kwenda kuthibitisha ubora wa bidhaa zao wanazozalisha.

"Hakikisheni mnaendelea kuzalisha bidhaa zenye ubora unaokubalika kila siku na sio leo mnapata leseni na cheti na baada ya hapo msianze kutengeneza bidhaa zisizokuwa na ubora tutakuwa tunapita na kuwafanyia ukaguzi wa mara kwa mara, kwani sheria inaturuhusu kufanya hivyo," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Ihnemeter, ambayo inazalisha na kuuza vifaa vya umeme ikiwamo Meter, Abraham Rajakili, aliishukuru TBS kwa kuwapatia vyeti na leseni za ubora kwani huo ni mwaga mzuri wa kuingia sokoni kwa kukubalika zaidi na kujiamini.

# NEC yaombwa wakalimani lugha ya alama Oktoba

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imeombwa kuweka wakalimani wa lugha ya alama kwenye vituo vyote 80,155 vya kupigia kura katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28 mwaka huo.

Imeelezwa kuwa hatua hiyo itasaidia kuimarisha dhana ya demokrasia na haki ya ushiriki wa watu wenye ulemavu wakiwamo viziwi katika uchaguzi huo.

Ombi hilo lilitolewa jana mkoani Mtwara na Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), Farida Selemani, alipokuwa akifungua mafunzo ya siku moja kwa wasimamizi wasaidizi 18 wa uchaguzi kutoka majimbo yote 10 ya mkoani humo.

Mafunzo hayo yaliyofanyika mjini hapa, yalitolewa na CHAVITA Mtwara na kufadhiliwa na Foundation For Civil Society.

Alisema katika kuimarisha dhana ya demokrasia na haki ya ushiriki wa watu wenye ulemavu wakiwamo wenye ulemavu wa kusikia na kundi maalumu kwa ujumla katika masuala ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 , CHAVITA tawi la mkoa wa Mtwara kimedhamiria kutoa elimu na kufanya mazungumzo ya ushawishi kwa wasimamizi hao wa mamlaka ya uchaguzi ili kufahamu haki ya walemavu katika uchaguzi.

Selemani alisema kwa kuwa kiziwi ana ulemavu wa kutosikia na wakati mwingine anakuwa na tatizo la kuongea, hivyo inakuwa vigumu kuwasiliana nao kwa njia ya kuongea na njia bora ya kuwasiliana nao ni kwa kutumia lugha ya alama, hivyo kuna kila sababu kwa Tume katika hatua zote za uchaguzi kuwa na wakalimani wa lugha ya alama ili viziwi na wao waweze kushiriki kikamilifu katika uchaguzi mkuu.

"Tume iweke wakalimani wa lugha ya alama kwenye vituo vya kupigia kura...njia nyingine ni kwa kutumia maandishi ya ishara au michoro ya lugha ya alama ambayo itasaidia kwa wale ambao wanajua kusoma na kuandika," alisema na kuongeza:

"Kwa kufanya haya, watu wenye ulemavu wataweza kupata fursa pana ya kushiriki katika uchaguzi mkuu na kuchagua viongozi wanaowapenda."

Akitoa mada kwa wasimamizi hao, mwezeshaji wa mafunzo hayo, Selemani Nahatala, alisema katika mkataba wa kimataifa kuhusu haki za watu wenye ulemavu wa mwaka 2006 ibara ya 29 umeweka wazi kuwa ushiriki wa masuala ya kisiasa na kijamii watu wenye ulemavu wana haki sawa kama ilivyo kwa watu wengine ambao sio walemavu.

# EXIM yataja sababu kupata faida licha ya janga la corona

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim imetangaza kupata ongezeko la faida (kabla ya kodi) kwa asilimia 35 katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka kilichoisha mwezi Juni 30, mwaka huu, huku ikieleza sababu zilizochangia.

Imeeleza kuwa mafanikio hayo yametokana na ufanisi kiutendaji licha ya changamoto za kiuchumi kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jijini Dar es Salaam na Ofisa Mkuu wa Fedha wa benki hiyo, Shani Kinswaga, benki hiyo imefanikiwa kupata faida ya Sh. bilioni 6.58 katika robo ya pili ya mwaka huu ikilinganishwa na faida ya Sh. bilioni 4.90 kwa kipindi kama hicho mwaka uliopita.

"Tunafurahi kuripoti matokeo mazuri kwa robo ya pili ya mwaka wa fedha 2020 licha ya athari kubwa ya janga la COVID-19 kwenye uchumi. Tumerejesha asilimia 8 kwenye mfuko wa wanahisa. Tunayachukulia mafanikio haya kama chachu ya kuendelea kufanya vizuri ili kutimiza malengo yetu na ya wateja wetu," alisema.

Aidha, alibainisha kuwa benki hiyo imeshirikiana kikamilifu na sekta zilizoathirika zaidi kiuchumi kutokana na janga la COVID-19 katika kuhakikisha sekta hizo zinajikwamua kwenye changamoto ya kifedha baada ya kuathirika na janga hilo.

Juni 2020, benki ya Exim ilitoa msamaha wa zaidi ya Sh. bilioni 160 kwa njia ya likizo ya malipo na upanuzi wa vipindi vya ulipaji wa mikopo ili kusaidia wateja wa benki hiyo ambao biashara zao zilizoathirika zaidi na athari za kiuchumi za COVID-19.

"Jumla kuu ya mali zetu zote imebaki kuwa Sh. trilioni 1.8, ikichangiwa hasa na ongezeko la asilimia 3 ya amana za wateja wetu katika kipindi hiki cha robo ya pili ya mwaka, hivyo kufanya jumla ya amana zote za wateja wetu kuwa Sh. trilioni 1.33. Aidha, shughuli zetu nchini Tanzania, Comoro na Uganda zote zimerekodi ukuaji wa amana za wateja wakati wa robo hii," aliongeza.

Kinswaga alibainisha: "Benki imerekebisha mkakati wake wa muda wa kati (Medium Term Plan) kufuatia changamoto ya COVID-19 kwa lengo la kuendeleza kasi ya ukuaji. Mkakati huo unategemea 'rasilimali watu, mchakato na teknolojia' katika kukuza ukuaji endelevu. Matokeo ya robo hii ni ushahidi wa maendeleo yaliyofanywa."

Katika kipindi hicho cha robo mwaka, Benki ya Exim ilizindua kampeni yake mpya 'Maliza Kirahisi Kidigitali' inayolenga kuhamasisha wateja wa benki hiyo kutumia zaidi huduma za kidigitali ili kurahisisha upatikanaji wa huduma zinazotolewa na benki hiyo sambamba na kuokoa muda ambao wangeutumia kufuata huduma hizo kwenye matawi ya benki hiyo.

Alisema kampeni hiyo ilikuja kipindi ambacho jamii inapitia mabadiliko kuelekea huduma za kidigitali hususani katika huduma za kifedha na manunuzi, hali iliyochochewa zaidi mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona.

# NMB yatenga bil.1.9/- ujenzi wa maghala

**Na Happy Severine,** SIMIYU

BENKI ya NMB mwaka huu imetenga Sh. bilioni 1.9 zitakazotumika kwa ajili ya kujenga maghala ya kuhifadhia mazao eneo ambalo serikali imesema linahitaji mchango wa taasisi za fedha nchini.

Ufadhili huo ulibainishwa mwishoni mwa wiki na Kaimu Ofisa Mkuu wa Fedha wa benki hiyo, Benedicto Baragomwa, alipokuwa anatoa maelezo kwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alipotembelea banda la benki hiyo kabla ya ufunguzi rasmi wa maonyesho ya Nanenane ambayo mwaka huu yanafanyika kitaifa mkoani Simiyu.

Mkoa wa Simiyu umekuwa mwenyeji wa maonyesho hayo kitaifa tangu mwaka 2018 na Benki ya NMB imekuwa mmoja wa wafadhili wake wakubwa na mwaka huu imechangia Sh. milioni 42.5 kuyafanikisha.

Katika maelezo yake kwa Makamu wa Rais, Baragomwa pia alisema NMB imeanza kusambaza na kuuza bima kwa wakulima kupitia huduma yake ya NMB Bancassurance ambayo imejipatia umaarufu mkubwa sokoni kutokana na thamani yake kubwa ya fedha kwa wateja.

Makamu wa Rais alisema serikali imeanzisha bima ya mazao itakayowafidia hasara watakayopata wakulima kutokana na ukame, uharibifu na uvamizi wa wadudu, mafuriko na majanga mengine.

Ofisa huyo alisema huduma za bima ambazo mpaka sasa hivi zinatolewa na benki hiyo kwa wakulima ni pamoja na bima za hali ya hewa, bima ya mazao yalioko shambani, bima za moto na wizi (kwa mazao yaliyohifadhiwa) na bima kwa ajili ya vifaa vya kilimo.

Huku akizitaka benki nchini kuongeza ukopeshaji wakulima ambao sasa hivi ni asilimia tisa tu ya mikopo yote, Samia alizitaka benki kujikita pia kwenye ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya kilimo. Alizipongeza taasisi hizo kwa ushiriki wao katika Nanenane ya mwaka huu na mchango wake katika jitihada za kukifanya kilimo nchini kuwa cha kisasa.

"Natambua umuhimu wa ushiriki wenu kwenye maadhimisho haya kwa kuwa nyie (benki na sekta binafsi kwa ujumla) ndiyo chachu ya kukua kwa kilimo chetu kwa kushirikiana na serikali katika kutekeleza maeneo ya kipaumbele ya kuongeza uzalishaji na tija kwenye kilimo," alisema Makamu wa Rais.

Akiwa kwenye banda la NMB, kiongozi huyo aliahidiwa na Baragomwa kuwa taasisi benki hiyo itaendelea kushirikiana na Serikali ya Awamu ya Tano kuwawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi pamoja na kuwaletea maendeleo Watanzania wote kwa ujumla kupitia huduma zake mbalimbali za kisasa zikiwamo zile za kidijitali

Katika maelezo yake kwa Makamu wa Rais, Baragomwa alibainisha mambo kadhaa ambayo benki hiyo imeyafanya katika kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano za kujenga uchumi imara kupitia kilimo na ufugaji ikiwamo kutenga Sh. bilioni 1.9 kwa ajili ya ujenzi wa maghala.

Alisema tangu mwaka 2016, Benki ya NMB imetoa zaidi ya Sh. bilioni 800 kusaidia kilimo na mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo. Na ndani ya miaka miwili, imefungua akaunti 500,000 za wakulima zikiwamo 86,000 za wakulima wa pamba wa Simiyu zilizofunguliwa mwaka huu.



Kaimu Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa, akipokea vitabu vyenye mwongozo wa mafunzo ya lishe bora kwa wakulima na mwongozo wa kitaifa wa uongezaji wa virutubisho kibaiolojia katika mazao ya chakula kutoka kwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, wakati wa uzinduzi wa maonyesho ya Nanenane kitaifa katika viwanja vya Nyakabindi, mkoani Simiyu mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Halmashauri yakabiliwa uhaba madarasa 1,297

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, inakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 1,297, kati ya vyumba 2,334 vinavyohitajika katika shule za msingi zilizoko katika halmashauri hiyo.

Akipokea vyumba viwili vya madarasa vilivyojengwa na Shirika la World Vision Tanzania Kanda ya Kagera katika Shule ya Msingi Ruzila na nyumba ya walimu katika Shule ya Msingi Karama Kata ya Rukoma, Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri hiyo, Devotha Mwesiga, alisema vyumba vya madarasa vilivyopo sasa ni 1,037.

"Serikali inafanya kila jitihada kuhakikisha inaboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, na ndiyo maana inashirikiana kwa karibu na mashirika yanayosaidia kuboresha miundombinu ya shule ili kuhakikisha wananchi wanapata elimu itakayowasaidia kujiinua kiuchumi," alisema.

Mwakilishi wa Meneja wa World Vision Kanda ya Kagera, Magembe Petro, alisema ujenzi wa miundombinu hiyo ulianza baada ya kutembelea shule hizo na kujionea uhitaji uliokuwa ukizikabili.

"Tulipotembelea Shule ya Msingi Ruzila kabla ya kujengewa vyumba viwili vya madarasa, baadhi ya wanafunzi walikuwa wakisomea kwenye darasa lililojengwa kwa udongo na fito, sasa tunawakabidhi madarasa haya mawili, nina imani watasoma kwa raha," alisema.

Alisema ujezi wa vyumba hivyo viwili vya madarasa umegharimu shilingi milioni 56 na nyumba ya walimu imegharimu shilingi milioni 69.5.

Mmoja wa walimu wa Shule ya Msingi Karama, Leina Malichades, alisema ujenzi wa nyumba hiyo ya walimu utamsaidia kupunguza changamoto ya kutembea umbali mrefu wa takriban kilomita 14 kwenda kazini.

"Gharama za maisha zilikuwa juu kutokana na kulazimika kutumia usafiri wa bodaboda karibia kila siku kwenda kazini na kurudi nyumba, sasa nitaanza kuishi jirani na shule, hii pia itasaidia kufanyika kwa maandalizi mazuri ya kufundisha," alisema.

Nipashe
Spotika




WACHEZAJI 10-BORA WA EPL MSIMU WA 2019-20 UK. 12&13




## ISIKUPITE

MABAO mawili Pierre-Emerick Aubameyang aliyofunga kwenye mechi ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Chelsea juzi, yanamfanya kufikisha jumla ya mabao 13 kwa Arsenal kwa mwaka 2020 tu. Mchezaji pekee aliyefikisha idadi hiyo mwaka huu kwa klabu za England ni Said Benrahma, ambaye amecheka na nyavu mara 14 akiichezea Brentford kwenye Championship.




# NYOTA BORA WATANO WALIONOGA NA RONALDO

**TURIN,** Italia

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Cristiano Ronaldo, muda wote wa uchezaji wake umepambwa na mafanikio makubwa huku akibeba mataji mengi na tuzo nyingi binafsi.

Alitarajiwa kupata mengi zaidi wakati wa msimu huu 2019-20 kule Turin akiwa na Juve, na ameshabeba taji lake la pili la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kwa msimu wake wa pili. Na bado wapo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Wachezaji gani bora zaidi kuwahi kucheza na Ronaldo?

Makala haya yanakuchambulia nyota bora zaidi watano waliokipiga na nyota huyo wa kimataifa wa Ureno.

### 1. KARIM BENZEMA

Mengi yamesemwa kwa kipindi cha miaka miwili tangu Ronaldo aondoke Real, lakini Karim Benzema alijitolea na kubeba mikoba ya Mreno huyo ambaye alicheza naye.

Hakuna mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi na Cristiano Ronaldo kuliko Benzema, ambapo amecheza naye jumla ya mechi 342, wakati wawili hao kwa pamoja wametengeneza mabao 76 kwa kila mmoja kwa kipindi cha karibia muongo mmoja waliocheza pamoja.

Benzema ndiye amebeba majukumu ya Real baada ya Ronaldo, licha ya awali kucheza kama mshambuliaji wa kati wakati alipojiunga nao mwaka 2009.

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Ufaransa tangu kuondoka kwa Ronaldo yeye ndiye amekuwa nguzo ya mabao ya kikosi hicho.

### 2. MESUT ÖZIL

Ozil na Ronaldo walifurahia maisha ya soka wakati wakicheza pamoja kwa kipindi cha miaka minne.

Ozil ndiye mchezaji ambaye Ronaldo hakutaka auzwe kutoka Real Madrid mwaka 2013. Wawili hao walicheza kwa ushirikiano mzuri zaidi, nyuma ya Benzema na walitengeneza mabao mengi kwa pamoja.

Mabao 38 katika mechi 149 yalikuwa ya kuvutia wakati akiwa kwenye jezi ya Real kuanzia mwaka 2010 hadi 2013. Özil alikuwa injini ya kuwatengeneza mashambulizi washambuliaji akitokea kwenye kiungo ya kati, kabla ya kuhamia winga ya pembeni.

Kaka, Angel di Maria, Gonzalo Higuain pia walikuwa miongozi mwa wafungaji wa mabao kwa usaidizi wake, huku ubunifu wa Luka Modric ulikuja hapo mwaka 2012 kwa ajili ya kuimarisha mashambulizi.

### 3. GARETH BALE

Majeraha ya mara kwa mara yalimfanya Bale kutokuwa na mechi nyingi za kucheza pamoja na Ronaldo. Kwa pamoja walitengeneza mabao 41 katika mechi 157 walizocheza pamoja.

### 4. MARCELO

Uvumi kuhusu majaliwa ya Marcelo pale Real Madrid ulimfanya ahusishwe na uwezekano wa kwenda Juventus mwaka jana ili akajiunge na rafiki yake wa karibu, Cristiano Ronaldo.

Hilo halikushangaza. Kwani ni Benzema na Sergio Ramos ndio wachezaji pekee waliocheza mechi nyingi (339) kwa pamoja na Ronaldo wakati wa kipindi chao cha uchezaji.

Mabao 25 kati ya 33 ya Ronaldo na Benzema yalichangiwa na Marcelo.

### 5. WAYNE ROONEY

Orodha hii inakamlilishwa na Wayne Rooney ambaye alicheza na Cristiano Ronaldo wakati wa umri wao wa ujana.

Wakati wakicheza pamoja kule Manchester United, Ronaldo alikuwa akicheza zaidi kama winga wa kulia na Rooney - ambaye ajiunga na 'Mashetani Wekundu' hao akitokea Everton, alicheza kama mshambuliaji wa kati.

Wawili hao kwa jumla walitengeneza mabao 25 kwa kipindi cha miezi 18 ya mwanzo wakicheza pamoja, wote walikuwa vijana wadogo.

Hata hivyo, haraka mambo yakabadilika na wakajikuta wakicheza kama washambuliaji patina baada ya Ruud van Nistelrooy kuondoka mwaka 2006. Rooney alitoa pasi za mwisho 11, huku Ronaldo akitoa 14 kati yao.

Extra Time

# WACHEZAJI 10-BORA WA EPL MSIMU WA 2019-20



JAMIE VARDY

**LONDON,** England

MSIMU wa Ligi Kuu ya England (EPL) 2019-20, umemalizika kwa kuweka rekodi ya kucheza kwa kipindi cha miezi 11. Soka lilisimamishwa Ulaya na kwingineko kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, na msimu ukasimama kwa miezi mitatu na nusu.

**Tangu kurudi kwa EPL mwezi uliopita, kumekuwa na mambo ya kuvutia na mengine ya utata. Hatimaye Liverpool walitwaa taji la Ligi ya England kwa mara ya kwanza baada ya miaka 30, huku mbio za kuwania kumaliza kwenye nne bora zikiwa za kuvutia na timu nyingine zikafanikiwa kubaki Ligi Kuu siku ya mwisho.**

Chelsea na Manchester United walijiunga na Liverpool pamoja na Manchester City kumaliza kwenye nne bora baada ya mechi 38. Norwich City ilishuka daraja, ikifuatwa na Bournemouth na Watford.

Liverpool ikiwa chini ya Jurgen Klopp, ilimaliza ligi kwa kujikusanyia pointi 99 baada ya mechi 38.

Makala haya yanachambua orodha ya wachezaji 10-bora walionyesha kiwango cha kuvutia zaidi msimu huu...

### #10. BRUNO FERNANDES | MAN UNITED

Usajili wa Januari wa Bruno Fernandes ulileta mchango mkubwa mno kwa kikosi cha Manchester United. 'Mashetani Wekundu' hao walikuwa nje ya nne bora kabla ya ujio wake na mchango wake umeisaidia timu hiyo kwa kiasi kikubwa kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kiungo huyo raia wa Ureno alileta pumzi mpya kwa kikosi cha Ole Gunnar Solskjaer na kuwawezesha kumaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi, yeye akiwa katikati na kuiongezea nguvu timu hiyo.

Fernandes amecheza mechi 14 za Ligi Kuu kwa Manchester United tangu alipoanza kuichezea Februari. Kwa kifupi maisha yake mafupi nchini England kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, yamemfanya atikise nyavu mara nane na kutwaa tuzo ya mchezaji bora wa mwezi mfululizo.

Kiungo huyo wa zamani wa Sporting, amekuwa moja ya usajili bora zaidi wa Januari katika historia ya hivi karibuni ndani ya kikosi cha Man United, atakuwa msaada mkubwa kwa siku za usoni katika kikosi hicho.

### #9. DANNY INGS | SOUTHAMPTON

Danny Ings hatimaye alimaliza kusumbuliwa na majeraha na kufurahia msimu akiwa na Southampton. Mchezaji huyu wa England amekipaisha kikosi cha kocha, Ralph Hasenhuttl na kumaliza katika nafasi ya 11 kwenye msimamo, huku yeye akitikisa nyavu mara 22 kwa jina lake.

Akijulikana kwa kutochoka na kujituma sana uwanjani, Ings alikuwa akifunga mabao mara kwa mara kwa 'Watakatifu' hao na kujiweka kwenye nafasi kubwa ya kuitwa katika kikosi cha England cha kocha, Gareth Southgate.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alikuwa na kazi ya kuvutia mno kwenye safu ya ushambuliaji na ameisaidia zaidi Southampton.

### #8. TRENT ALEXANDER-ARNOLD | LIVERPOOL

Trent Alexander-Arnold haraka sana amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa wachezaji wa kuvutia zaidi katika soka la kisasa.

Akiwa ametoa pasi za mwisho 12 msimu uliopita na kuweka rekodi ya kuwa na pasi za mwisho nyingi kwa mlinzi katika Ligi Kuu ya England kwa msimu mmoja, Alexander-Arnold msimu huu alifikisha 'asisti' 13.

Kwa nyongeza, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, pia alifunga mabao manne, yakiwamo aliyofunga nyumbani na ugenini dhidi ya Chelsea na kuendelea kujitambulisha yeye mwenyewe kama mmoja wa walinzi bora wa kulia duniani.

### #7. PIERRE-EMERICK AUBAMEYANG | ARSENAL

Pierre-Emerick Aubameyang alikuwa mmoja wa wachezaji walioisaidia zaidi Arsenal msimu huu. Raia huyo wa Gabon alifurahia mafanikio binafsi kwa kufikisha mabao 22 kwenye Ligi Kuu.

Hata hivyo, mabao yake hayakuisaidia Arsenal kupata nafasi ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa msimu ujao, kwani timu ilimaliza ligi katika nafasi ya nane nyuma ya timu kama Leicester City na Wolves, lakini ameibeba kutwaa Kombe la FA juzi kwa mabao yake mawili wakati wakishinda 2-1 dhidi ya Chelsea kwenye fainali iliyopigwa Uwanja wa Wembley, hivyo kufuzu moja kwa moja kucheza Ligi ya Europa msimu ujao.

Aubameyang pia alishinda tuzo ya Kiatu cha Dhahabu msimu uliopita, lakini safari hii alipitwa bao moja na Jamie Vardy aliyefunga 23. Nahodha huyo wa Arsenal ni mmoja wa washambuliaji bora zaidi kwenye EPL kwa sasa na amekuwa na mchango mkubwa kwa kikosi hicho cha Mikel Arteta.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 31, bado hajasaini mkataba mpya na klabu hiyo na imeripotiwa kwamba anaweza kusaini ndani ya wiki chache zijazo.

### #6. MOHAMED SALAH | LIVERPOOL

Maisha ya Mohamed Salah pale Liverpool yalikuwa na mafanikio ya haraka sana ya kuvutia. Akiwa ametwaa tuzo ya Kiatu cha Dhahabu katika misimu yake miwili ya kwanza England, nyota huyo wa Misri, aliikosa tuzo hiyo msimu huu baada ya kutikisa nyavu mara 19 tu.

Hata hivyo, Salah alikuwa na mchango mkubwa kwa 'Wekundu' hao wakati wakimaliza ligi kwa kutwaa ubingwa wa EPL kiaina yake. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, alitoa pasi za mwisho 10.

Salah alicheza mechi 34 za EPL kwa kikosi hicho cha Klopp, huku akitengeneza upatina mzuri na Roberto Firmino na Sadio Mane.

### #5. JAMIE VARDY | LEICESTER CITY

Jamie Vardy alikuwa na msimu wa kuvutia na mwenye mafanikio binafsi wakati akiisaidia Leicester City kumaliza nafasi ya tano kwenye msimamo. Muingereza huyo aliondoka na tuzo ya Kiatu cha Dhahabu msimu huu baada ya kuibuka mfungaji bora kwenye Ligi Kuu, ikiwa ni kwa mara ya kwanza katika maisha yake ya soka, baada ya kufunga mabao 23.

Kwa nyongeza, Vardy amekuwa mchezaji wa kwanza mwenye umri mkubwa zaidi katika historia ya EPL kutwaa tuzo hiyo, akiizima ile iliyowekwa na Didier Drogba. Katika umri wake wa miaka 33, namba tisa huyo wa Leicester hajaonyesha ishara ya kushuka kwa makali yake.

### #4. SADIO MANE | LIVERPOOL

Sadio Mane alifurahia mmoja wa msimu wake bora zaidi katika maisha yake ya soka, wakati alipocheza na kuwa nguzo muhimu ya Liverpool kipindi ikibeba taji. Hivyo, mara zote, Mane ni mtu wa matukio makubwa, akiwa amefunga mabao 18 na kutoa pasi za mwisho tisa.

Akiwa ametwaa tuzo ya Kiatu cha Dhahabu kwa pamoja na Aubameyang na Salah msimu uliopita, raia huyo wa Senegal msimu huu alifunga mabao chini ya 20 kwenye EPL.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, alikuwa na mchango mkubwa kwa safu ya ushamabuliaji ya Klopp katika misimu ya hivi karibuni.

### #3. VIRGIL VAN DIJK | LIVERPOOL

Akiwa anachukuliwa kama mlinzi bora zaidi wa kati duniani kwa sasa, Virgil van Dijk amekuwa mchezaji wa tano kwenye historia ya Ligi Kuu ya England kucheza katika kila dakika wakati wakitwaa taji la EPL msimu huu.

Nyota huyu wa kimataifa wa Uholanzi alikuwa muhimili mkubwa wa safu ya ulinzi ya Liverpool. Akiwa amemaliza nafasi ya pili mwaka 2019 katika tuzo ya Ballon d'Or nyuma ya Lionel Messi, Van Dijk aliendelea kuwa imara zaidi kwa msimu huu.

Msimu uliopita, alikuwa mlinzi wa kwanza kushinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa EPL tangu John Terry alivyoibeba mwaka 2005.

Van Dijk kwa muda mfupi aliocheza Liverpool amejiimarisha mwenyewe kama mmoja wa walinzi bora zaidi kuwahi kucheza kwa vijogoo hao.

### #2. JORDAN HENDERSON | LIVERPOOL

Baada ya miaka ya kuibuka kwa maswali juu ya uwezo wake na nafasi yake ya unahodha, hatimaye Jordan Henderson akafikia umri wa kufurahia mafanikio yake. Alikuwa nguzo kubwa kwa Liverpool wakati ikitwaa Kombe la Ligi Kuu ya England kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 30.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, amekuwa nahodha wa kwanza kwa kipindi cha miaka 30 kunyanyua makwapa na kuliinua Kombe la Ligi Kuu ya England.

### #1. KEVIN DE BRUYNE | MAN CITY

Licha ya utawala wa Liverpool kwenye Ligi Kuu ya England, Kevin de Bruyne alikuwa na msimu wa kuvutia zaidi kama mchezaji na kujiimarisha vizuri sana kwenye safu ya kiungo.

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Ubelgiji uwezo wake wa kutengeneza na kufunga mabao, mara zote ulimfanya kuwa muamuzi wa mechi nyingi za Manchester City msimu huu.

De Bruyne aliifikia rekodi ya Theirry Henry ya kufikisha pasi za mwisho 20 kwa msimu mmoja na alifunga mabao 13 kutokea kiungo wa kati.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, huu ulikuwa msimu wake bora zaidi katika kipindi chake cha kucheza soka.

## Nukuu

"Nafikiri Robert Lewandowski amekuwa na msimu wa kuvutia sana katika maisha yake ya soka, bahati mbaya tuzo ya Ballon d'Or imefutwa, kitu ambacho si sawa. Hii si sawa kabisa kwa Bayern na Robert Lewandowski," **Mwenyekiti wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge akiamini kuwa huu ulikuwa mwaka wa Lewandowski kutwaa Ballon d'Or kama tuzo hiyo isingefutwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, COVID-19.**



"Sifikirii kuhusu mwisho, lakini naota. Ndoto ni huru na mara zote naona kwamba nitaipa mataji Villarreal, unatakiwa kufurahia kila wakati unaokuja mbele yako. Hapa ukiwa na Villarreal, naona kabisa kwamba nahitaji kutwaa mataji," **Kocha wa zamani wa Arsenal, Paris Saint-Germain na Sevilla, Unai Emery baada ya kusaini mkataba wa kuinoa Villarreal ya Hispania.**



"Uwezekano wa kuwapo kwenye kikosi chetu ni mdogo sana, maana inaonekana wazi kabisa kwamba nafasi hiyo ni ngumu kwake. Lakini kama kuna miujiza basi inawezekana tukawa naye katika kikosi chetu kwa ajili ya mchezo huu wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atalanta," **Kocha wa Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel akizungumzia kumkosa Kylian Mbappe katika mechi hiyo itakayopigwa Agosti 12, mwaka huu.**






Baadhi ya wachezaji wa Lipuli FC ya Iringa wakifanya mazoezi kabla ya moja ya mechi za Ligi Kuu kwenye Uwanja wa Samora Iringa. **PICHA: MAKTABA**

# SIRI TIMU TANO KUSHUKA DARAJA LIGI KUU NI HII

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE timu tano zimeshuka daraja, hatutoziona tena Ligi Kuu, badala yake tutazionа zikicheza Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara msimu ujao.

**Timu hizo ni Singida United ambayo yenyewe ilishuka mapema sana, na timu za Lipuli FC, Ndanda na Alliance ilibidi zisubiri mechi za mwisho kabisa, kabla ya kuungana na kufunga safari kwenda Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara, lakini Mbeya City ilipo nea mechi ya mchujo kwa kuitoa Geita juzi wakati Mbao FC wenyewe walitolewa na Ihefu FC hivyo nayo kuaga Ligi Kuu.**

Singida United imeteremka daraja ikiwa imeambulia pointi 18 tu kwenye mechi zake 38 ilizocheza ikishika nafasi ya mwisho ya 20, na ilitabiriwa mapema tu kuwa ingeshuka.

Ikiwa nyumbani, Lipuli ililazimishwa kushuka daraja kwa lazima na Yanga, ilipochapwa bao 1-0 kwenye uwanja wake wa nyumbani, Samora mjini Iringa na mechi ilipomalizika tu, ilijikuta ikiwa kwenye nafasi ya 18 na pointi zake 44, ikilazimika kuteremka.

Ndanda FC nayo imeshuka daraja baada ya kukubali kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya Mbao FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba mjini Mwanza, hivyo kubakia na pointi zake 41, ikishika nafasi ya 19 ambayo ni ya mwisho kutoka mkiani huku wababe wao hao wakifuzu kucheza mechi ya mchujo dhidi ya Ihefu FC.

Alliance FC, pamoja na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Namungo kwenye Uwanja wa Nyamagana mjini Mwanza, bado haukuiwezesha kubaki Ligi Kuu, nayo ikashuka moja kwa moja, ikimaliza na pointi 45, lakini ikiwa kwenye nafasi ya 17.

Ni kwa nini timu hizi zimeshuka daraja msimu huu? Mwandishi wa makala haya anachambua...

## SINGIDA UNITED

Msimu huu ilikuwa hoi bin-taabani kipesa, lakini kiuongozi. Ilipanda mwaka 2017 na kuanza kucheza rasmi Ligi Kuu msimu wa 2018/19, ikiwa moja ya timu tishio kiasi cha kupewa nafasi ya kushiriki hata michuano ya SportPesa.

Ilisajili wachezaji mahiri kutoka Uganda, Kenya, na hata Zimbabwe. Ilikuwa na uwezo pia wa kuwapeleka kwa mkopo wachezaji wengine akiwamo Feisal Salum alisajiliwa na Singida United, halafu akapelekwa Yanga.

Katika hali ya kushangaza, msimu huu ilionekana kabisa kuwa haiko kama ilivyokuwa na haikuwashangaza watu wengi kushuka daraja baada ya kudumu kwenye Ligi Kuu kwa misimu miwili tu.

## NDANDA FC

Kuna usemi unaosema kuti la mazoea limemuangusha mgema. Ndanda FC ilizoea karibu kila msimu kuponea kushuka daraja kwenye mechi za mwisho kabisa.

Tangu ilipoanza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2014/15, timu hiyo yenye maskani yake mkoani Mtwara imekuwa ikicheza kwa kujiokoa kushuka daraja zaidi kila msimu.

Na kwa bahati mbaya imekuwa ni timu inayojipapatua kwenye dakika za mwisho, lakini badala ya kujifunza kutokana na makosa ikawa kama imezoea hali hiyo. Mbaya zaidi kwao msimu huu mechi ya mwisho ikaenda kumalizia ugenini badala ya nyumbani, tena na timu ya Mbao FC ambayo nayo ilikuwa inasaka ushindi kufa au kupona ili isishuke hivyo kujikuta ikichapwa 2-0 na kuhitimisha maisha ya misimu sita ikiwa Ligi Kuu Tanzania Bara.

## LIPULI FC

Hakuna shabiki yeyote wa soka aliyetarajia kuwa timu ya Lipuli FC ingeshuka daraja msimu huu. Ni kwa sababu ilianza ligi vizuri tu ikifanya vema kwenye mechi zake za mwanzo hadi mzunguko wa kwanza ulipomalizika.

Ni pale baadhi ya wachezaji walipoanza kugoma kwa kudai stahiki zao, wakiongozwa na straika wao hatari, Paul Nonga ndipo timu ilipoanza kusuasua.

Pamoja na hayo, iliendelea kucheza Ligi Kuu na wachezaji waliopo. Sidhani hata kama viongozi wa Lipuli na mashabiki wa mkoani Iringa kwenye maskani ya klabu hiyo, kama walifikiria kuwa itashuka.

Hata msimamo wa Ligi Kuu, mechi moja kila timu kabla ligi kumalizika, bado Lipuli ilionekana haiko kwenye hatari kubwa. Ilikuwa iko juu ya zote. Matokeo ya kufungwa na Yanga, pia Mtibwa kushinda mabao 2-1 dhidi ya Ruvu Shooting, yalipa mkono kwa heri timu hiyo kwa mshangao wa wengi.

## ALLIANCE FC

Kilichoiponza Alliance ni uwiano mdogo wa mabao ya kufunga na kufungwa kwani ilimaliza ikiwa na pointi 45, kama Mbao FC na Mbeya City, tofauti na timu za Mbao FC na Mbeya City zilizoangukia mechi za mchujo. Naweza kusema, timu za Simba na Azam FC ndizo zilizoishusha Alliance daraja.

Kipigo cha mabao 5-1 dhidi ya Simba ilichopata siku chache kabla ligi kumalizika na kisha kuchapwa 5-0 nyumbani kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza dhidi ya Azam, tayari iliifanya iwe na idadi kubwa ya mabao ya kufungwa. Kumbuka hata kwenye mzunguko wa kwanza nyumbani, Alliance ilichapwa mabao 4-1 dhidi ya Simba. Ni mechi ambazo ziliifanya kuwa na uwiano mbaya wa mabao ya kufunga na kufungwa kwani ilikuwa imefunga mabao 36 na 48 ya kufungwa, na kama ukiondoa mabao hayo 14, Alliance ingeenda kwenye mechi za mchujo, kwani imeshuka kwa hasi 12, wakati Mbao iliyotolewa na Ihefu juzi kwa faida ya bao la ugenini, yenyewe ilikuwa na hasi 10.

## MBAO FC

Tayari hapo juu maelezo yake yanajitosheleza, lakini kosa kubwa ililolifanya Mbao ni kuruhusu mabao 2-0 ugenini ilipocheza dhidi ya Ihefu FC mechi ya kwanza ya mchujo.

Hata hivyo, ikarejea tena makosa juzi katika mchezo wa marudiano kwa kuruhusu kufungwa mabao mawili wakati ikishinda 4-2 nyumbani, CCM Kirumba, hivyo ikaaga rasmi Ligi Kuu.

**JE, WAJUA?**



KWA mabao 23, aliyofunga Jamie Vardy msimu huu akiwa na umri wa miaka 33, na kutwaa Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu England, yanamfanya kuwa mchezaji wa kwanza mwenye umri mkubwa zaidi katika historia ya EPL kutwaa tuzo hiyo, akiizima ile iliyowekwa na Didier Drogba.



## HABARI DODOMA

# Jumuiya za CCM Dodoma zapewa jukumu kura za urais

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Dodoma kimezitaka jumuiya zake kuhakikisha mkoa huo unaongoza kwa kura nyingi za urais kama ilivyokuwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Maelekezo hayo yalitolewa mwishoni mwa wiki na Kaimu Katibu wa CCM, Mkoa huo, Pili Mbaga, katika kikao cha Baraza la Jumuiya ya Wazazi ya CCM iliyokutana kwa ajili ya kuchagua mwakilishi wa jumuiya hiyo katika nafasi ya ubunge viti maalum.

Alisema Jumuiya ya Wanawake wa CCM (UWT) na Jumuiya ya Vijana wa CCM (UVCCM), zina wajibu wa kuhakikisha zinalinda historia ya kuongoza kwenye kura za urais kwa kuhamasisha watu wote waliojiandikisha kupiga kura kujitokeza kupiga kura kwa wingi.

"Niwaombe wazazi tunaenda kwenye uchaguzi mwezi Oktoba tunatakiwa tujipange ili Rais John Magufuli apate kura nyingi kama ilivyokuwa mwaka 2015, pia tuhamasishe kura nyingi kwa wabunge wetu na madiwani, tunahitaji ushindi wa kishindo," alisema.

Alisema baada ya kumaliza kura za maoni wanapaswa kujipanga kupata ushindi wa kishindo kwa kuwa safari bado ndefu.

"Tukirudi huko tujue majukumu yetu sisi jumuiya ni kwenda kufanya kazi ya kuhakikisha chama kinashinda, tunajua nyie wazazi hamna tabia ya kukengeuka, tuhakikishe zinapatikana kura za kutosha," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa huo, Damas Mukasa, alisema watahakikisha wanatimiza lengo hilo.

Aliwahimiza wanachama wa CCM na wajumuiya hiyo kuendelea kuzingatia maadili na kutojihusisha na vitendo vya rushwa.

"Suala la rushwa halikubaliki, niendelee kuwaasa wagombea wote wa nafasi mbalimbali na hata kwenye chaguzi nyingine tuendelee kuwa waadilifu," alisema.

Alisisitiza jumuiya hizo kufanya kazi kwa kushirikiana kwa kuwa nguvu ya chama hicho ipo kwenye jumuiya hizo.

Katika kuchaguzi huo, Egla Mamoto aliibuka mshindi kwa kura 36 kati ya 39 zilizopigwa huku mgombea mwenzake Ernajoyce Halo akipata kura tatu.



Meneja wa takwimu, ufuatiliaji mradi na tathmini wa mradi wa 'The Challenge Initiative – Tupange Pamoja' unaotekelezwa na Shirika la Jhpiego, Charles Mushi (kulia), akiwasilisha mada kwenye kikao kuhusu mkakati wa kuanzisha mradi huo jijini Dodoma, na kuutambulisha kwa kamati za afya Mkoa na Jiji, kilichoongozwa na Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Best Magoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mavunde ataka maombi ya uchaguzi mkuu

**Na Peter Mkwavil,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, amewaomba Watanzania kuliombea Taifa katika kipindi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu Oktoba 2020, ili liendelee kuwa na amani na mshikamano.

Mavunde alitoa ombi hilo jana alipokuwa akipokea msaada kwa niaba ya wajane, wazee na watu wanaoishi katika mazingira magumu wapatao 200 ambao wanalelewa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Kata ya Chang'ombe Jiji la Dodoma uliotolewa na Taasisi ya Dar-Ul- Muslimeen. Alisema Watanzania wanawajibu wa kumuomba Mungu ili wapitishwe viongozi watakaotokana na chaguo lake, ambao watashikamana kwa upendo mkubwa na kuilinda amani iliyopo.

Aidha, alisema serikali itaendelea kutambua mchango mkubwa unaofanywa na taasisi na kampuni binafsi kwa kusaidia misaada mbalimbali kwa jamii ya watu wenye mahitaji wa kielimu, afya, chakula na mavazi.

"Nitoe rai kwa taasisi na kampuni za watu binafsi ziige mfano kwa taasisi ya Dar-ul-Musilmeen chini ya Mkurugenzi wake Mzee Bhanji, ambaye mara zote amekuwa akijitoa kwa ajili ya kusaidia watu wenye mahitaji, lakini sivyo hivyo tu hata watu wenye mishahara mikubwa na kipato wanaweza wakafanya hivyo," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Muslimu Bhanji alisema kuwa msaada huo umetolewa kwa ajili ya kuwasaidia jamii isiyojiweza wa kata hiyo ya Chang'ombe ili kutatua kero zinazowakabili.

Naye, Mwenyekiti wa BAKWATA Wilaya ya Dodoma, Bashiru Husseni, alisema kuwa sadaka iliyotolewa na taasisi hiyo kwa jamii inayolelewa na BAKWATA ni mbuzi wapatao 50 wenye thamani ya Sh. milioni tatu kwa ajili ya wajane, wazee na wanaoishi katika mazingira magumu.

Aliwaasa walengwa waliopewa sadaka hiyo kuitumia kwa malengo yaliyokusudiwa na wasiuze ili kujipatia fedha kwa kuwa wakifanya hivyo watakwenda kinyume na mapenzi mema kwa taasisi iliyowasaidia.

# TASAF yaiomba jamii ushirikiano kutambua kaya wenye uhitaji

**Na Mwandishi Wetu,** BAHI

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), umeitaka jamii kushirikiana na serikali kuwatambua wananchi wenye uhitaji ili kuondoa udanganyifu katika utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF III) awamu ya pili unaotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mtaalamu wa Utafiti na Maendeleo wa TASAF, Tumpe Lukongo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutoa mafunzo kwa wakuu wa idara na wawezeshaji wa ngazi ya Halmashauri ya Wilaya ya Bahi kuhusu uhakiki wa kaya maskini.

Lukongo alisema TASAF III awamu ya kwanza imeisha na sasa wapo katika utekelezaji wa TASAF III awamu ya pili, ambapo kwa sasa wanafanya uhakiki wa wanufaika ili kupata masjala safi ya walengwa kabla ya kuanza utekelezaji wake.

"Rais John Magufuli wakati anazindua TASAF III awamu ya pili alituelekeza kwamba kabla hatujaanza utekelezaji tufanye uhakiki na kusafisha daftari la kaya maskini ili tuwapate walengwa wanaostahili, na tulishaanza kutekeleza maelekezo hayo nchi nzima na sasa tunamalizia mkoa wa Dodoma, Singida, Kigoma, Lindi na Mtwara," alisema.

Alisema ili suala hilo lifanikiwe ushirikiano kati ya wananchi na serikali katika ngazi zote ni muhimu kinyume na hapo jitihada za serikali za kuondoa umaskini zinaweza zisifikiwe kwa walengwa.

"Jamii ndio inamjua mtu maskini, inamjua mtu anayehitaji msaada zaidi ya wengine, hivyo ikishirikiana na serikali kwa ukweli na uwazi itasaidia kuondoa changamoto ya udanganyifu ambayo imekuwapo katika baadhi ya maeneo," aliongeza.

Alisema lengo la uhakiki huo ni kuwa na orodha halisi ya walengwa kwenye masjala ya kaya za walengwa kwa kuondoa waliofariki, aliyehama, kiongozi wa kijiji, kaya ya mjumbe wa kamati ya usimamizi wa jamii na kaya ambayo haikufika kuchukua malipo yake mara mbili mfululizo.

Kadhalika, alisema wameboresha dodoso la utambuzi na namna ya udodosaji ambapo mwanzo walikuwa wanatumia wahusika ngazi ya jamii lakini kwa sasa wanatumia wawezeshaji ngazi ya halmashauri ambao wanapewa uelewa na kutumia vishkwambi kuingiza taarifa badala ya makaratasi.

Aidha, alitaja mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa TASAF III awamu ya kwanza kuwa ni pamoja na maisha ya walengwa kuboreka, walengwa wengi kujishughulisha na shughuli za kuongeza kipato, kupata uwezo wa kusomesha watoto wao, kuboresha afya na lishe.





# NEC yawafunda wasimamizi wa uchaguzi mkuu

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imewataka maofisa walioteuliwa na kusimamia uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu, kuepuka kufanya vitendo ambavyo vinaweza kuvuruga uchaguzi huo.

Hayo yalisemwa juzi jijini Mbeya na Kamishna wa Tume hiyo, Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mary Longway, alipokuwa anafungua mafunzo ya siku tatu kwa wasimamizi wa uchaguzi wa Mkoa wa Mbeya.

Jaji Longway aliwataka maofisa hao kufuata sheria na maelekezo yanayotolewa na tume hiyo badala ya kufanya kazi hiyo kwa mazoea na bila kuzingatia masharti hali ambayo inaweza kusababisha kuvurugika kwa mwenendo wa uchaguzi huo.

Alisema maofisa hao hawatakiwi kufanya jambo lolote ambalo litakuwa tofauti na maelekezo ya tume, kanuni na Katiba ya nchi ambayo ndiyo sheria mama.

"Pamoja na kwamba baadhi yenu ni wazoefu kwenye usimamizi wa uchaguzi, lakini natoa wito kwenu kuepuka kufanya kazi hiyo kwa mazoea, mkazingatie yale mtakayoelekezwa na tume," alisema Jaji Longway.

Akiwaapisha maofisa hao, Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Mbeya, Zawadi Laizer, aliwataka kuwa waadilifu na wenye kutenda haki kulingana na kiapo walichoapa.

Alisema uadilifu wa mtu ndio unaompa ujasiri wa kuapa kiapo chochote na kukisimamia na kwamba kwa mtu ambaye sio mwadilifu anaweza akajikuta wakati wowote anachukuliwa hatua kwa sababu ya kukiuka kiapo chake.

"Kiapo ni mkataba wa kujifunga, ni kwamba unakubali kuwa pale utakapokiuka jambo lolote linalohusiana na uchaguzi basi utapelekwa kwenye vyombo vya sheria kwa ajili ya hatua zaidi," alisema Zawadi.

Mafunzo hayo ya kwa wasimamizi wa uchaguzi kwa Wilaya za Mkoa wa Mbeya, yalianza juzi na yanahitimishwa leo ambapo maofisa hao watasimamia uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu ikiwa ni utekelezaji wa matakwa ya Katiba.

# Viwanja vyote vya Nanenane kupimwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeagiza viwanja vyote vinavyotumika kwa ajili ya Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) nchini kupimwa na kupatiwa hatimiliki ili wamiliki waanze kulipia kodi ya pango la ardhi kwa mujibu wa sheria ya za nchi.

Agizo hilo lilitolewa juzi jijini Mbeya na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alipokuwa anafungua maonyesho ya wakulima Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo yanafanyika katika Uwanja wa John Mwakangale.

Alisema wamiliki wa viwanja hivyo wamekuwa wakiyatumia baadhi ya maeneo ya viwanja hivyo kibiashara na wanakusanya mapato, lakini serikali hainufaiki chochote kutokana na mapato hayo ambayo wanakusanya.

Aliwaagiza makamishna wa ardhi wa mikoa yote ambayo viwanja hivyo vya maonyesho vipo, waanze mara moja kupima na kutoa hati miliki huku akisisitiza kuwa hata yeye atawasaidia kupata hati hizo.

"Huu uwanja nimeambiwa unamilikiwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole na una ukubwa wa ekari 27, hiki mnafanyia biashara maana nimeona risiti pale mlangoni watu wanalipia, kwa hiyo lazima tuwapimie na mlipe kodi na nimeelekeza viwanja vyote vya aina hii nchini vipimwe na vianze kulipiwa," alisema Lukuvi na kuongeza.

"Tutawaachia yale maeneo ambayo mnayatumia kufundishia wananchi bila malipo, lakini haya ambayo mnafanyia biashara lazima mlipie maana kuna maeneo humu watu wanafanyia biashara mwaka mzima," aliongeza.

Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema wamepokea maelekezo ya Waziri, na kwamba na yeye atawasilisha taarifa hiyo kwa viongozi wake wa kitaifa kwa ajili ya utekelezaji.

Alisema baada ya kuwasiliana na mabosi wake, taasisi hiyo itashirikiana na Halmashauri ya Jiji la Mbeya pamoja na mkoa kupitia kwa kamishna wa ardhi kutekeleza agizo hilo.

"Hilo ni agizo ambalo tunatakiwa tulitekeleze, mimi kama kiongozi wa kituo nahakikisha leo leo (juzi), nitawapigia simu viongozi wangu ili tuanze utekelezaji.

Katika hatua nyingine, Lukuvi alizitaka taasisi za utafiti na makampuni yanayouza pembejeo kuhakikisha zinasambaza kwa wananchi teknolojia zinazobuniwa ili ziwasaidie wakulima kuzalisha kwa tija zaidi.

Alisema baadhi ya kampuni zilibuniwa za kuuza pembejeo za kilimo kwa ajili ya kupata ruzuku ya serikali na kwamba baada ya ruzuku hizo kuondolewa, kampuni hizo zilitoweka na sasa hazionekani kwenye biashara.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema pamoja na kwamba mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inaongoza kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali, lakini bado wakulima hawazalishi kwa tija inayotakiwa kutokana na teknolojia kuwa ya chini.

Alisema ili kuhakikisha maonyesho hayo yanakuwa na tija kwa wananchi ni lazima kila kiongozi awahamasishe wananchi kwenye eneo lake ili wazitumie teknolojia zinazoonyeshwa kwenye maonyesho hayo.

Chalamila alisema serikali inaendelea na harakati za kuboresha miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege ili kuwarahisishia wakulima usafirishaji wa mazao yao.

Maonyesho hayo kitaifa yanafanyika katika Mkoa wa Simiyu na kwa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yanafanyikia jijini Mbeya huku yakiwa na kaulimbiu isemayo 'Kwa Maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Chagua Viongozi Bora 2020'.



Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo (mwenye tai nyekundu), akikata utepe kuzindua mkakati maalumu wa mkoa huo, kukabiliana na mimba za utotoni, ulioasisiwa Februari mwaka huu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Dawa ujenzi barabara zisizo na viwango yaja

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imenunua gari lenye mashine ambayo itakuwa na kazi ya kuhakiki kiwango na ubora wa barabara kabla ya kukabidhiwa. Lengo la hatua hiyo ni kuondoa tatizo la ujenzi wa barabara zisizokuwa na viwango.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi, Isaack Kamwelwe, wakati akikagua ukarabati wa barabara kuu ya Tanzania na Zambia (Tanzam), eneo la Mabadaga Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya.

Kamwelwe alisema tayari gari hilo lenye mashine ya kupima ubora wa barabara nchini limeagizwa na kwamba hadi kufikia mwezi Septemba itaanza kufanya kazi ya kukagua viwango vilivyojengwa.

"Tumekuja na teknolojia mpya ya kuhakiki viwango vya ubora katika barabara zetu nchini, mashine hizo ambazo zitakuwa na data zitatoa majibu endapo zimekidhi vigezo vya ubora unaohitajika ili zikataliwe au zikubaliwe kabla ya viongozi kuzindua," alisema Kamwelwe.

Alisema mashine hiyo itakuwa mwarobaini wa kumaliza tatizo la ujenzi holela wa barabara nchini kwa madai kuwa zinajengwa kwa gharama kubwa lakini hazidumu zinaharibika.

Katika kuhakikisha ujenzi wa barabara nchini unazingatiwa mameneja wa TANROADS mikoa ya Singida na Mwanza wameagizwa kusimamia vyema ujenzi wa barabara kwenye maeneo yao badala ya kuridhika na kukamilika na muda mfupi kuharibika tena.

Alimpongeza Meneja wa TANROADS Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Eliazary Rweikiza, kwa ukarabati wa barabara kwenye maeneo mengi ya mkoa huo ambayo yaliathiriwa na mvua za masika.

Katika hatua nyingine Waziri Kamwelwe ametoa siku saba kwa TANROADS Mkoa wa Mbeya kuweka alama za pundamilia kwenye eneo la Mabadaga na Malenga ili kuwasaidia wanafunzi kuvuka kwa usalama.

Mhandisi Rweikiza alisema wataendelea na zoezi la kukarabati barabara zote za mkoa huo ambazo ziliharibiwa na mvua, na kwamba hadi sasa baadhi ya barabara za Kyela, Chunya, Mbarali na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya zimekarabatiwa kwa kiwango kinachotakiwa.

Alisema watakahakikisha barabara zote zilizoharibika kwa sababu ya mvua zinatengenezwa na zirejee kwenye hali yake ya kawaida ikiwamo na madaraja.



# ZEC yatumia bil. 1.2/- vitambulisho vya mpigakura

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) imetumia Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya utengenezaji wa vitambulisho vipya vya kupigia kura na Sh. milioni 240 kwa ajili ya ugawaji wa vitambulisho hivyo.

Akizungumza na waandishi wa habari, mkurugenzi wa uchaguzi wa Tume hiyo, Thabit Idarous Faina, alisema vitambulisho 566,352 vimezalishwa kwa ajili ya wapigakura katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Faina, alisema kati ya vitambulisho hivyo 272,115 ni vya wanaume na 294,237 ni vya wanawake.

Alisema kwa Wilaya ya Kaskazini 'A' vitambulisho vilivyozalishwa vilikuwa 62,117 Kaskazini 'B' vitambulisho 40,237, Wilaya ya Kati Unguja vitambulisho 51,644 na Kusini Unguja ni 28,985.

Wilaya ya Magharibi 'A' alisema vitambulisho vilivyozalishwa ni 62,701, Wilaya ya Magharibi 'B' ni 70,159 na Mjini ni 109,009.

Mkurugenzi huyo alisema kwa Pemba, Wilaya ya Wete vimetengenezwa vitambulisho 37,195, Wilaya ya Micheweni, 26,586, Chakechake, 42,933 na Mkoani, 34,786.

Hata hivyo, alisema kwa wale wasiokuwa na sifa za kupigia kura, Tume inaendelea kupokea taarifa mbalimbali kwa watu waliofariki hadi pale ZEC itakapofunga daftari la kudumu la wapigakura siku saba baada ya uteuzi wa wagombea. Alisema tume itaendelea kutatua changamoto ya upatikanaji wa vitambulisho kwa wananchi ambao bado hawajaenda kuchukua na kuwataka kufika katika ofisi za Tume za wilaya ili waweze kuchukua vitambulisho vyao na kupata haki yao ya msingi ya kikatiba ya kupiga kura.

"Yeyote ambaye amehakiki na ana vitu vinavyostahiki ikiwamo risiti basi atapatiwa kitambulisho kabla ya siku ya kura katika uchaguzi wa mwaka huu kufanyika," alisema.

Alisema kuwa tume ilipitia hatua mbalimbali za uchaguzi ikiwamo kuanza rasmi uandikishaji wa wapigakura wapya na uhakiki wapigakura waliokuwamo kwenye daftari la kudumu la wapigakura Januari 18, mwaka huu, katika Wilaya ya Micheweni Pemba na kumalizika rasmi Machi 4, mwaka huu.

Zoezi hilo kwa mara ya pili lilifanyika katika mikoa yote ya Unguja na Pemba kuanzia Mei 30 hadi Juni 12, mwaka huu uwekaji wazi wa taarifa za wapigakura ulioanza Julai 8 hadi 14, mwaka huu na ugawaji wa vitambulisho vya kupigia kura wananchi walioandikishwa katika daftari la kudumu la kupigia kura Julai 18 hadi 20 kwa Pemba na Julai 26 hadi 27 kwa kisiwa cha Unguja.



Mkurugenzi wa Huduma Binafsi na Shule ya Sabato Jimbo la Kusini Mashariki wa Kanisa la Wasabato, Mchungaji Sadikiel Shehemba (kulia) na viongozi wengine wa kanisa hilo Mbezi Luis Dar es Salaam, wakivishwa skafu na vijana wa Chama cha Watafutanjia (Pathfinder) wa kanisa hilo, kabla ya ufunguzi wa wiki ya sikukuu ya makambi (camp meeting) uliofanyika juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waliochaguliwa watakiwa kutosahau majukumu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa CCM Mkoa wa Mjini kichama, Talib Ali Talib, amewataka viongozi wa Umoja wa Wazazi waliochaguliwa kutosahau kutekeleza majukumu yao ya kazi ili kurudisha imani kwa waliowachagua.

Alisema kuna baadhi ya viongozi wanatumia nguvu nyingi wakati wa kutafuta madaraka, lakini wanawakimbia wapigakura wake jambo ambalo linasababisha kudhoofisha nguvu za chama hicho.

Aliyasema hayo wakati akifungua kikao cha Baraza Kuu la Wazazi Mkoa wa Mjini cha kuchagua mbunge na mwakilishi wa viti maalum wa mkoa huo kupitia Umoja wa Wazazi huko Amani.

Aliwataka wajumbe hao kuchagua viongozi wenye nidhamu, heshima na mapenzi ya wananchi wao ili waweze kuleta mabadiliko katika chama na serikali.

Aliwaagiza viongozi wa umoja huo kufanya kazi kwa bidii ili kufikia malengo ya CCM ya kupata ushindi katika ngazi zote.

Naye Msimamizi Mkuu wa Uchaguzi huo ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Marina Joel Thomas, alisema mchakato wa kuchagua kiongozi atayekiwakilisha chama hicho katika uchaguzi mkuu bado unaendelea hivyo si vyema walioongoza katika kura za maoni kusherehekea.

Kwa upande wao wagombea ambao kura zao hazikutosha kuongoza katika uchaguzi huo wameahidi kushirikiana na walioshinda ili CCM iendelee kushika dola na kuwatumikia wananchi hususan wa kipato cha chini.

# Dk. Mwinyi aahidi kushirikiana na taasisi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MJUMBE wa Taasisi ya Al Miraaj, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ataendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali nchini ambazo zimekuwa zikisaidia wananchi.

Kauli hiyo aliitoa wakati akikabidhi msaada wa nyama iliyotolewa na taasisi hiyo kwa wananchi wasiojiweza wa Masingini Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja kwa ajili ya Sikukuu ya Eid Hajj.

Dk. Mwinyi ambaye ni mgombea wa Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), alisema endapo atakuwa Rais wa Zanzibar ataendeleza uhusiano huo ili walio wengi waweze kunufaika na misaada hiyo.

"Taasisi hii imekuwa ikinisaidia wakati nilipokuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani na hata kule bara Jimbo la Mkuranga, hivyo naahidi ushirikiano wetu utaendelea ili kuona wanaendelea kutoa misaada kwa wananchi wetu," alisema.

Aliishukuru jumuiya hiyo kutoa sadaka kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar wasiojiweza nao waweze kusherehekea sikukuu kama watu wengine.

"Naamini walio wengi katika eneo hili watafaidika na sadaka hii kwa kuwa taasisi hii inatusaidia sana sisi kutupatia misaada mbalimbali kwa ajili ya wananchi wetu," alisema. Aliziomba taasisi nyingine zenye uwezo kuendelea kusaidia ili waweze kupata radhi za Mwenyezi Mungu.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Tanzania, Sheikh Arif Yussuf Abdul-rahman, alisema, lengo la msaada huo ni kusaidia wananchi mbalimbali wakiwamo yatima, watu wenye ulemavu na makundi mengine. Alisema ni kawaida ya taasisi hiyo kuchinja na kutoa misaada mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania wanyonge ili waweze kupata kitoweo kwa ajili ya sikukuu.

Aliahidi kuendelea kutoa misaada hiyo katika maeneo mbalimbali ya Tanzania na kuziomba taasisi nyingine kujenga utamaduni wa kutoa misaada kwa wasiojiweza ili waweze kupata radhi za Mwenyezi Mungu.

Sheikh Othman Maalim, aliwasisitiza Waislam wenye uwezo kuchinja katika kipindi cha Sikukuu ya Eid Hajj kwa kuwa ni ibada kubwa mbele ya Allah.

"Kuchinja mnyama kama kondoo, ngamia, mbuzi, ng'ombe katika kipindi hiki ni sunna na thawabu kubwa mbele ya Allah siku ya kiama hasa kuwapa maskini," alisema.

Jumla ya ng'ombe 100, mbuzi 100 na ngamia watatu walichinjwa kwa ajili ya sadaka ya sikukuu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI.

**DIAMOND RAHIM KARMALI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 728 AHF TOYOTA LANDCRUISER.** Chassis namba **HZJ800009643.** Engine namba **IHZ0053043.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi: Taarifa ya Polisi: **DAR/SEL/RB/565881/2020.**

115840302

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ESCON KACHELE**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA SHENLY YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 418 ARJ.** KWA YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI **KAH//RB/255/2020.**

115840402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA –MWANZA**

**SHAURI NA 30 LA 2020**

**SIXTUS LULENGA KAHI.................................... MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **FRENK THOMAS MARWA**
2. **NATIONAL MICROFINANCE BANK PLC**
3. **TANZANIA POSTAL BANK.................................WADAIWA**

**KWA: FRENK THOMAS MARWA**

Unafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua shauri/ombi dhidi yako katika baraza la ardhi na nyumba mkoa wa mwanza, ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 03/08/2020 katika chumba cha baraza, barabara ya posta jengo liko mkabala na mahakama kuu ya biashara, Tanzania.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria
KAA ukijua kwamba kushindwa kufika, baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.
Imetolewa nami kwa Amri na chapa ya baraza leo tarehe 29/07/2020

MASAO
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
MWANZA

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BENALD FRANCIS MAKOLE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA LAND CLUSER PRADO YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 164 CSB** YENYE CHASIS NO **VZJ950057766** NA ENGINE **NO SV20313036** KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI: **KAH/RB/272/2020.**

215840702


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# GGML, NEEC zawezesha kupata zabuni

**Na Mwandishi Wetu**

WAJASIRIAMALI nchini wameanza kujengewa uwezo kwa ajili ya kupata zabuni mbalimbali.

Hatua hiyo imetokana na kampuni ya uchimbaji wa madini ya Geita (GGML) kwa kushirikiana na Baraza la Kitaifa la Uchumi na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), ikusaini makubaliano ya utekelezaji wa programu maalumu ya kuwajengea uwezo wafanyabiashara mkoani Geita kushiriki kikamilifu katika zabuni zinazotolewa na mgodi huo.

Makubaliano hayo yaliyotiwa saini Julai 20, mwaka huu mkoani Geita, yatadumu kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi Juni 30, mwaka 2021.

Rais wa GGML, Simon Shayo, alisema progamu hiyo pia inalenga kuwajengea uwezo wazabuni wa Mkoa wa Geita ili kuweza kutambua na kuzingatia viwango na ubora wa bidhaa na huduma zinazohitajika katika shughuli za GGML.

Aliongeza kuwa programu hiyo pia inalenga kuwaunganisha wazabuni wa GGML na mamlaka mbalimbali za serikali, sekta binafsi na jamii kwa ujumla zinazotoa fursa zinazowezesha kushiriki kikamilifu katika zabuni hizo.

"Programu hii itawawezesha wazabuni wa GGML kupata soko la uhakika la bidhaa na huduma wanazozalisha hivyo kujiongezea kipato cha mtu mmoja mmoja, kipato cha kaya na jamii kwa ujumla hivyo kuchangia pato la Taifa kwa upande mmoja," alisema.

Aidha, alisema GGML itaweza kupata huduma na bidhaa zenye ubora kutoka kwa wazabuni wa ndani zitakazoongeza tija kwa wazalishaji wa ndani.

"GGML tumejitolea katika maendeleo endelevu ya jamii inayotuzunguka. Tunapenda kuacha urithi, hata wakati madini yatakapokuwa yameisha kuchimbwa. Kusudi letu ni kuongeza ushiriki wa Watanzania kwenye shughuli za mgodi ili tuweze kusaidia jamii ambayo tunafanya nayo kazi," alisema Shayo.

Shayo alifafanua kuwa GGML inajivunia kuwa walipa kodi bora na wakubwa nchini ambapo mwaka 2019 pekee, jumla ya kodi iliyolipwa na GGML kwa serikali ya Tanzania ilikuwa takriban Sh. bilioni 467 sambamba na kutoa ajira kwa Watanzania zaidi ya 5,000.

Akizungumza katika uzinduzi wa program hiyo, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Uwekezaji), Dorothy Mwaluko, alisema programu hiyo imetengenezwa wakati mwafaka.

"Itahakikisha changamoto ambazo zinafanya kampuni za kitanzania kushindwa kupata zabuni kwenye uwekezaji unaofanyika nchini, zinatatuliwa na kumwezesha mwekezaji kutekeleza kikamilifu sheria za nchi kwa kununua bidhaa na kutumia huduma za Watanzania zinazokidhi viwango.

"Nipende kuwapongeza GGML kwa kukubali kuwezesha programu hii kwa kuwa wafanyabiashara watakaonufaika na mafunzo haya mbali na kushiriki shughuli za uzalishaji katika mgodi huu, pia yatawafungulia njia kushiriki katika miradi inayotekelezwa kwenye sekta zingine," alisema.

Aidha, Katibu Mtendaji wa NEEC, Beng'i Issa, alisema uzinduzi wa programu hii unabebwa na kauli mbiu isemayo "Ushiriki na Ushindani wa Uwazi katika Kukuza Uchumi".

Alisema kauli mbiu hiyo inajielekeza katika kujenga uwezo kwa wafanyabiashara wa ndani ili wapate fursa ya kushiriki katika sekta ya madini.



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Uwekezaji), Dorothy Mwaluko (kulia), akikabidhi mkataba wa makubaliano ya utekelezaji wa programu maalumu ya kuwajengea uwezo wafanyabiashara mkoani Geita kwa Makamu wa Rais wa Kampuni ya GGML, Simon Shayo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# RITA yaanzisha huduma kimtandao

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

SERIKALI imewataka wananchi kuchangamkia huduma zinazotolewa na Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) kwenye Maonyesho ya Wakulima Nanenane, yanayofanyika wilayani Simiyu ambayo ni muhimu kwenye maisha yao.

Ofisa Habari wa RITA, Grace Kyasi, alisema kuwa huduma zao zinagusa maisha ya kila Mtanzania katika nyanja tofauti kama vile elimu, ajira, afya, mikopo ya elimu ya juu, ndoa, wosia na mirathi.

Alisema jamii inahitaji kufahamu huduma za RITA haziepukiki kutokana na kugusa maisha ya kila siku katika jamii.

"Kwa mfano; mtoto anapozaliwa atahitaji kupata cheti cha kuzaliwa, mtu anapofariki ndugu watahitaji kufuatilia cheti cha kifo cha marehemu, pia watu wanapofunga ndoa wanatakiwa kusajili vyeti vyao vya ndoa na vilevile tuna huduma ya kuandika na kuhifadhi wosia pamoja na usimamizi wa mirathi," alisema Grace.

Alitaja huduma nyingine zitolewazo na RITA kuwa ni usajili wa talaka, usajili wa bodi za wadhamini pamoja na kuasili watoto.

Alisema, wakala pia umeanzisha huduma ya usajili wa vizazi na vifo na uhakiki wa vyeti kwa njia ya mtandao na mtu anaweza kuipata popote alipo nchini.

"Katika kufikiria kusogeza huduma zetu karibu na wananchi, wakala umeanzisha huduma ya usajili wa vizazi na vifo kwa njia ya mtandao popote ulipo, unaojulikana kama "E- Huduma" inapatikana katika tovuti ya Wakala ambayo ni www.rita.go.tz." Alisema.

Alisisitiza wananchi kutumia huduma zake ili ziwafaidishe katika mahitaji yao mbalimbali na kuwakaribisha kutembelea banda lao namba 94.

# Kiluvya wamlilia JPM malipo ya fidia

**Na Beatrice Shayo**

WANANCHI wa eneo la Kiluvya, Mwanalugali na Chalinze wamemwomba Rais John Magufuli kuwasaidia ili wapatiwe malipo ya fidia kutokana na kucheleweshwa kwa zaidi ya miaka mitano.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wananchi hao waliopitiwa na mradi wa umeme unaotoka Dar es Salaam hadi Chalinze, walieleza kuwa walifanyiwa tathmini na kujulishwa watalipwa fidia tangu mwaka 2015.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wenzake wa Kiluvya, Narin Wolper (70), alisema kilio chao ni kikubwa na kwamba kuanzia mwaka 2015 walitathminiwa na kuelezwa kuwa nyumba zao zitavunjwa ili kupisha mradi huo na kujulishwa malipo watapatiwa kwa wakati.

"Kama mimi na umri wangu nyumba yenyewe haijaisha hata madirisha hakuna, kwa hiyo wadudu wanaingia ndani na nyumba zetu zinabomoka, hatuwezi kufanya maboresho kwa kuwa wametueleza tusiendeleze chochote tusubiri fidia na mpaka sasa hakuna," alisema Wolper.

Alisema wanamwomba Rais Magufuli aingilia kati jambo hilo ili wapate haki yao kwani hawajui wanalipwa shilingi ngapi.

"Kila siku ni mawazo, tunangoja leo tunasema labda kesho, lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea," alisema Wolper.

Naye katibu wa kamati ya wananchi wanaopisha mradi wa umeme huo, Enirisha Mshana, alisema mwaka 2015 maofisa wa Wizara ya Nishati na Madini kuwaeleza kuwa maeneo yao yatachukuliwa kwa ajili ya mradi.

Alisema wananchi walikubali kwa sababu ni mradi wa serikali wa maendeleo ya nchi i.

"Wanaopitiwa na mradi waliunda kamati ndogo kwa ajili ya kufuatilia malipo na waliahidiwa kulipwa ndani ya miezi sita, tumefuatilia maeneo mbalimbali kuanzia kwa Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa, Naibu Waziri wa Nishati na majibu walikuwa wanatuambia malipo yapo tayari kinachosubiriwa ni Wizara ya Fedha," alisema.

Mshana alisema waliendelea kusubiri, huku wakiishi katika mazingira magumu kwani wengine nyumba zao zimedondoka.

"Mpaka sasa hakuna taarifa ambayo ni sahihi inayokuja kwa wananchi kutoka ngazi ya juu, kwenye magazeti tunaona taarifa mradi upo kamili mara bajeti imetenga fedha... sasa hiyo fedha imepelekwa kwenye mradi gani?" Alihoji Mshana.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Kijiji cha Mwanalugali, Deodatus Rweyekaza, alisema Rais Magufuli ameshaeleza fedha ipo hazina, lakini kinachowashangaza kwa nini hawapatiwi fidia.

Emmanuel Bundala, mkazi wa Chalinze, alisema tangu walivyosimamishwa kufanya maendeleo kwa ajili ya kupisha mradi huo, amepata hasara kubwa kwa kushindwa kuendelea na shughuli zake za ufugaji.

Alisema alitumia fedha nyingi katika uwekezaji huo na kwa sasa mabanda aliyoyajenda yamebomoka baada ya kukaa kwa muda mrefu.

# MAROTTA: KUMSAJILI MESSI NI NDOTO




**MILAN,** Italia

OFISA Mtendaji Mkuu wa Inter Milan, Giuseppe Marotta kwa mara nyingine amemwagia maji ya baridi uvumi wa juu ya uwezekano wa kumsajili nahodha wa Barcelona, Lionel Messi, akisema kwamba hiyo ni "ndoto."

Messi ameendelea kuhusishwa na Inter, huku nyota huyo wa Barca akiripotiwa kutokuwa na furaha pale Camp Nou na anajiandaa kuondoka kwa miamba hao wa LaLiga mara tu mkataba wake utakapomalizika mwaka 2021.

Hata hivyo, Marotta amekanusha uvumi huo mara baada ya mchezo wa mwisho wa msimu huu wakati Inter ikiibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Atalanta.

"Lazima tuwe wakweli, ni ndoto. Zinafurahisha," alisema Marotta akiiambia Sky Sport Italia.

"Messi ni mchezaji ambaye ana mahusiano makubwa sana na Barcelona, sehemu ambayo nafikiri anamalizia soka lake pale. Hivyo, narudia kusema kwamba ni ndoto."

Inter imemaliza msimu huu wa 2019-20 kwa kupitwa pointi moja tu na mabingwa wa Juventus baada ya ushindi wao wa Jumamosi dhidi ya Atalanta.

Ashley Young alifunga bao la pili kwa shuti kali nje ya 18 baada ya mchezaji mwenzake, Danilo D'Ambrosio kuipa Inter bao la uongozi ndani ya sekunde 50.

# Pulisic, Azpilicueta waipa pigo Chelsea

**LONDON,** England

CHRISTIAN Pulisic na Cesar Azpilicueta hawataichezea Chelsea kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich baada ya kuumia Jumamosi kwenye fainali ya kipigo cha 2-1 kutoka kwa Arsenal.

Nahodha Azpilicueta aliumia nyama za paja dakika tano baada ya kusababisha penalti iliyofungwa na Pierre-Emerick Aubameyang.

Na Pulisic, mfungaji wa bao la Chelsea pale Wembley, pia alitolewa nje dakika nne kabla ya mapumziko.

Pedro pia naye aliumia bega na kocha Frank Lampard ameondoa uwezekano wa nyota hao kuwapo kwenye mchezo wa pili wa hatua ya mtoano wa 16-bora dhidi ya Bayern, ambapo Chelsea itangia kwenye mchezo huo ikiwa nyuma kwa mabao 3-0 baada ya kufungwa kwenye mchezo wa kwanza.

"Sijui muda gani majeruhi hayo yatamweka nje, lakini najua kwamba wameumia nyama za paja Azpi na Christian," alisema Lampard baada ya mchezo huo.

"Watamfanyia uchunguzi ndani ya siku chache zijazo. Kwa uhakika kabisa hawatakuwa fiti kwa wiki ijayo."

Pedro, ambaye aliwekewa mtungi wa hewa ya oxygen na kubebwa kwenye machela kuondolewa uwanjani, anatarajia kujiunga na Roma kwa uhamisho huru wakati mkataba wake na Chelsea utakapomalizika mwezi huu.

"Naamini atakuwa ameteguka bega, sijajua kwa uhakika bado," alisema Lampard wakati alipoulizwa hali ya mshambuliaji huyo.






# *Conte aibwatukia Inter Milan*

**MILAN,** Italia

KOCHA Mkuu wa Inter Milan, Antonio Conte amedai yeye na kikosi chake walipata "ulinzi mdogo" kutoka kwa klabu wakati akitoa shutuma kwa Nerazzurri hao.

Inter ya Conte ilimaliza msimu wa 2019-20 wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, ikiwa nafasi ya pili, ikipitwa pointi moja na mabingwa Juventus, baada ya ushindi wa 2-0 wa Jumamosi dhidi ya Atalanta.

Danilo D'Ambrosio na Ashley Young walifunga mabao hayo kipindi cha kwanza na kuiwezesha Inter kupata pointi 82 baada ya mechi 38, akifikisha sawa na zile alizoshinda Jose Mourinho msimu wa 2009-10 wakati akitwaa mataji matatu.

Hata hivyo, Conte - katika msimu wake wa kwanza pale San Siro - alitoa shutuma baada ya mchezo wa juzi na awalia alibainisha kwamba hatasita kuondoka Inter kama hawatakuwa na furaha.

"Tunatakiwa kuwapa sifa vijana, pointi 82 ni nyingi, ni nyingi na imeonyesha kuna kazi kubwa imefanyika vizuri," alisema raia huyo wa Italia akiwaambia waandishi wa habari.

"Lakini inahuzunisha, kwa sababu nimeshuhudia Inter ikitendewa ndivyo sivyo, kulikuwa na shutuma nyingi dhidi ya wachezaji pamoja na mimi, sikulipenda hilo na pia niliona ulinzi mdogo kutoka kwa klabu.

HABARI MICHEZO

# Arteta amshukuru Guardiola kubeba FA

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amemshukuru Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola baada ya Arsenal kuifunga Chelsea 2-1 kwenye fainali ya Kombe la FA na kubainisha kwamba, huo ni wakati bora zaidi katika maisha yake ya ukocha.

Arteta aliondoka kule Man City katika nafasi yake ya kocha msaidizi Desemba mwaka jana baada ya miaka mitatu akifanya kazi pamoja na Guardiola na kwenda kuchukua mikoba ya Unai Emery pale kwenye dimba la Emirates.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 38, amefurahia mafanikio ya msimu wake wa kwanza pale Arsenal, kwa kulibeba taji hilo Jumamosi katika Uwanja wa Wembley na kuifanya Arsenal kuweka rekodi ya kulibeba taji hilo kwa mara ya 14.

Na Arteta, ambaye amekuwa kocha wa kwanza wa Arsenal kushinda taji kubwa kwenye msimu wake wa kwanza tangu George Graham katika msimu wa 1986-87, haraka alimsifia Guardiola.

"Amekuwa mtu muhimu katika maendeleo yangu kama kocha," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Yeye ndiye shujaa wangu. Nisingeweza kukaa hapa bila yeye. Natakiwa kumshuruku yeye kwa wakati huu mzuri."


Arteta pia alimsifia Pierre-Emerick Aubameyang kwa kufunga mabao mawili baada ya kutoka nyuma kwa bao 1-0 lililofungwa na Christian Pulisic.

Raia huyo wa Hispania ambaye alisema ana imani Aubameyang atasaini mkataba mpya, alimsifia nahodha huyo kwa kiwango alichokionyesha kwenye mchezo huo.

"Mechi kubwa zinahitaji mchezaji mkubwa, alifanya hivyo kwenye nusu fainali na leo tena," alisema.

"Watu wamekuwa wakiulizia kama anaweza kufanya makubwa kwenye mechi kubwa na leo amefanya hivyo."

Arsenal ilimaliza nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England – ikiwa nafasi ya chini zaidi tangu msimu wa 1994-95 – lakini wamepata nafasi ya kucheza Ligi ya Europa msimu ujao baada ya ushindi huo dhidi ya Chelsea.






# IBRAHIMOVIC AWEKA REKODI MABAO SERIE A

**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic ameweka rekodi ya kuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kufikisha mabao 10 kwa msimu mmoja kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, baada ya kufunga dhidi ya Cagliari, Jumamosi.

Straika huyo wa Milan, ambaye klabu hiyo inajadiliana naye kuhusu kuongeza mkataba wake ili abakie pale kwenye dimba la San Siro, alifunga dakika ya 55 wakati kikosi chake hicho kikiibuka na ushindi wa mabao 3-0 baada ya penalti yake kuokolewa.

Ibrahimovic mwenye umri wa miaka 38 na siku 302, alifikisha mabao hayo 10 katika mechi 18 tu alizocheza, akiwa amejiunga na klabu hiyo Januari.

Milan ambayo imekuwa kwenye kiwango cha kuvutia, imefunga mabao mengi zaidi kuliko timu nyingine kwenye Ligi Kuu tano kubwa za Ulaya, tangu kurudi kwa ligi ya soka baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Milan imefunga jumla ya mabao 35, huku mchango mkubwa ukitoka kwa Ibrahimovic.

Ni Real Madrid pekee imepata pointi nyingi (31) moja zaidi ya Milan (30) katika Ligi Kuu tano bora Ulaya baada ya kurudi kwa msimu huu.

# *Immobile ampiku Messi, CR7 akiifikia rekodi ya Higuain*

**ROME,** Italia

CIRO Immobile ameifikia rekodi ya Gonzalo Higuain ya kufunga mabao mengi zaidi kwenye msimu mmoja wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, wakati alipofikisha mabao 36 na kushinda tuzo ya Kiatu cha Dhahabu Ulaya kwa msimu wa 2019-20.

Straika huyo wa Lazio alifunga kwenye ushindi wa 3-1 dhidi ya Napoli na kikosi hicho cha kocha, Simone Inzaghi kilimaliza kwenye nafasi ya nne katika msimamo wa ligi hiyo.

Immobile aliifikia rekodi hiyo iliyowekwa na Higuain msimu wa 2015-16 wakati mshambuliaji huyo wa Argentina alipokuwa akichezea Napoli.


Nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, alifurahia msimu wake kwenye ligi hiyo na alikuwa akikabiliana na upinzani mkubwa kutoka kwa Cristiano Ronaldo wa Juventus, ambaye hakucheza mchezo wa mwisho dhidi ya Roma.

Hiyo maana yake ni kwamba, Immobile amebeba tuzo mbili msimu huu, ya mfungaji bora wa Serie A na mfungaji bora wa ligi kubwa tano za Ulaya.

Immobile amewapiku nyota kama mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowski mwenye mabao 34, Ronaldo (31) na Lionel Messi (25).



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# AUBAMEYANG: NAFURAHIA FA TU, SIJUI HATIMA YANGU

●●● Leo ni furaha tuna kombe, ndio hivyo tu, Mikel Arteta anastahili ushindi huu, amefanya kazi...

**LONDON,** England

PIEERE-Emerick Aubameyang ameshinda Kombe la FA kwa Arsenal baada ya kufunga mabao mawili kwenye fainali iliyopigwa pale katika dimba la Wembley juzi, lakini amewaacha na sitofahamu mashabiki wa 'Washika-bunduki' hao kuhusu majaliwa yake.

**Straika huyo wa kimataifa wa Gabon alidondosha kombe hilo wakati wanashangilia, baada ya kuisaidia Arsenal kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Chelsea, akifunga yote mawili.**

Bao lake la kwanza alifunga kwa penalti na la pili alifunga baada ya kumzidi akili mlinzi, Kurt Zouma na kuubetua mpira kwa juu uliompita golikipa Willy Caballero na kujaa wavuni.

Alipoulizwa nini anachoweza kusema kuhusu majaliwa yake, hasa kwa kuwa mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu ujao, Aubameyang aliiambia BBC One: "Hakuna, leo ni furaha tuna kombe, ndo hivyo."

Ilikuwa siku ambayo Arsenal ilistahili ushindi huo, huku ikipata nafasi ya kucheza Ligi ya Europa msimu ujao.

"Tumefurahia leo. Tuna furaha," alisema Aubameyang. "Emi (golikipa Emiliano Martinez) analia. Hiyo inaonyesha namna gani amefurahishwa na mchezo huu pamoja na kombe."

Mikel Arteta alijiunga na Arsenal kama kocha mkuu Novemba mwaka huu, na Aubameyang alisifia mchango wake.

"Nafikiri anastahili ushindi huu. Nafikiri amefanya kazi kubwa na tuna furaha kuwa naye. Tunamfuata yeye," alisema nyota huyo mwenye umri wa miaka 31.

Akizungumzia bao lake la ushindi, Aubameyang alisema: "Zouma ananijua vizuri. Anajua kwamba mimi natumia mguu wa kulia, ndio maana nikasema sawa, nikafunga kwa mguu wa kushoto.

"Maana nilijua yeye atauangalia vizuri mguu wa kulia, na hakuwa na uhakika kama nitaweza kupiga mpira ule."

Ushindi huo wa Arsenal kwenye FA umewafanya kuweka rekodi ya kulibeba taji hilo mara nyingi zaidi, ikiwa hii ni mara ya 14.

## ZISIKUPITE

### CHELSEA WAMTAKA POPE

CHELSEA inajaribu kumsajili golikipa wa Burnley, Muingereza Nick Pope mwenye umri wa miaka 28, huku uvumi juu ya majaliwa ya Kepa Arrizabalaga mwenye miaka 25, ukiongezeka. ***(Star Sunday)***

### UNITED YAMULIKA MONACO

MANCHESTER United imeingia kwenye mazungumzo na mlinzi wa Monaco, Benoit Badiashile mwenye umri wa miaka 19, lakini wanakabiliwa na upinzani kutoka kwa Bayer Leverkusen na Real Madrid. ***(TF1 via Mirror)***

### SPURS WAMUWANIA DEENEY

KLABU ya Tottenham Hotspur wanafikiria uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Watford, Troy Deeney mwenye umri wa miaka 32. ***(Mail)***

### PALACE KUMSAJILI ISMAILA

CRYSTAL Palace wanaangalia uwezekano wa kumsajili straika wa Watford, Ismaila Sarr mwenye umri wa miaka 22 raia wa Senegal na wanaweza kumuuza mshambuliaji wao, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 27, raia wa Ivory Coast kwa pauni milioni 40. ***(Sun on Sunday)***

### SANCHEZ AWEKWA SOKONI

KLABU ya Manchester United inaitaka Inter Milan kulipa pauni milioni 15 kama inataka kumsajili moja kwa moja mshambuliaji Alexis Sanchez mwenye umri wa miaka 31, raia wa Chile. ***(Sunday Express)***

### MALDINI IMANI KWA ZLATAN

MKURUGENZI wa soka wa AC Milan, Paolo Maldini amesema anamuona mshambuliaji Msweden Zlatan Ibrahimovic mwenye umri wa miaka 38, kuwa sehemu ya kikosi hicho msimu ujao. ***(ESPN)***

### PSG OFA KWA ALCANTARA

KLABU ya Paris St-Germain inaandaa ofa kwa kiungo wa Hispania, Thiago Alcantara,29, na ipo tayari kufikia bei wanayoitaka Bayern Munich kwa ajili ya mchezaji huyo, ambaye pia anawaniwa na Liverpool. ***(Le10Sport)***

### CITY WAJITOSA KWA SERGI

MANCHESTER City wanawania kumsajili kwa mkopo nyota wa Barcelona, Sergi Roberto, 28, ambaye anaweza kucheza kama kiungo, mlinzi na winga, huku wakiwa tayari kumtoa beki wao wa pembeni, Eric Garcia, 19, kwenda kwa miamba hao wa Hispania. ***(Sport)***

### EVERTON YAMUWANIA JOSHUA

KLABU ya Everton inajaribu bahati yake kumsajili straika wa Bournemouth, Joshua King, 28 raia wa Norway kwa pauni milioni 15. ***(Sun on Sunday)***

### SMALLING, FEDERICO KUPISHANA

JUVENTUS inafikiria kumtoa Federico Bernardeschi, 26, kwa Manchester United kama sehemu ya mpango wao wa kutaka kumsajili mlinzi wa England, Chris Smalling mwenye umri wa miaka 30, kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Inside Futbol)***

### NEWCASTLE YAMTAKA ROGERIO

KLABU ya Newcastle United inawania kumsajili mlinzi wa kushoto wa Sassuolo, Rogerio mwenye umri wa miaka 22 raia wa Brazil. ***(Sky Italia)***

HABARI MICHEZO

## Simba Queens pointi 3 bingwa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' (pichani) amesema anahitaji kufanya vizuri katika mechi yao ijayo dhidi ya Baobab Queens ili kutangazwa mabingwa rasmi kabla ya ligi hiyo kumalizika.



Malkia wa Simba hao wanaongoza ligi hiyo wakiwa na alama 50 baada ya mechi 19 wakifuatiwa na JKT Queens na Alliance Girls zenye pointi 43 kila moja wakati huu ligi hiyo ikibakiza raundi tatu kabla ya kufikia ukingoni.

Hivyo, Simba Queens ambayo itaikaribisha Baobab Jumatano katika Uwanja wa Uhuru, endapo itashinda mchezo huo itatangazwa bingwa ikiwa imebakiza mechi mbili dhidi ya Alliance Girls na TSC Queens inayoshika nafasi ya pili kutoka mkiani kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 12.

"Naenda kufanyia kazi mchezo wa leo (juzi dhidi ya Tanzanite), tungecheza na timu yenye ushindani mkubwa hii mechi tungapata sare, lazima niwahimize kupambana kwani bado hatujawa mabingwa licha ya kwamba tukishinda mechi ijayo tuna uhakika wa kuwa bingwa," alisema Mgosi baada ya kushinda mechi hiyo kwa mabao 2-1.

## Mlandege mabingwa Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdalla, ZANZIBAR**

TIMU ya Mlandege FC imetwaa rasmi ubingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar msimu wa 2019/2020 baada ya timu iliyokuwa ipambane nayo katika mchezo wake wa mwisho, Jang'ombe Boys kutofika uwanjani.

Mlandege imefikisha alama 68, huku nafasi ya pili ikienda kwa timu ya Zimamoto yenye alama 67 na nafasi ya tatu ikishikwa na JKU yenye alama 65 katika msimo wa huo wa Ligi Kuu Zanzibar.

Mlandege FC imeweka historia ya kutwaa taji hilo mara ya saba huku ikianza kulipeba mwaka 1996, 1997, 1998, 1999, 2001, 2002 na msimu huu wa 2019/2020.

Aidha, ubingwa huo wa timu ya Mlandege msimu huu umezima ndoto kwa timu zinazomilikiwa na majeshi kuendelea kuushikilia baada ya kuutwaa kwa takribani miaka 10.

Kwa upande wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF) kupitia Mkurugenzi wa Mashindano wa shirikisho hilo, Ali Mohammed Ameir, alisema ZFF itatoa tarehe rasmi ya kukabidhi kombe kwa mabingwa hao pamoja na zawadi nyingine kwa washindi katika vipengele mbalimbali ambavyo kamati ya mashindano imeviweka.

# AZAM YAIPIKU YANGA KWA NIYONZIMA, LYANGA NAYE

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Azam FC imezidi kujiimarisha kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Bara baada ya juzi kukamilisha usajili wa nyota wa kimataifa aliyekuwa akihusishwa sana na Yanga, Mnyarwanda, Ally Niyonzima, kwa kumsainisha mkataba wa miaka miwili.

Usajili huo umekamilika ikiwa ni siku mbili tangu Azam ilipoinasa saini ya kiungo Awesu Awesu aliyemaliza mkataba na Kagera Sugar.

Aidha, jana pia kiungo mshambuliaji wa Coastal Union ya Tanga, Ayoub Lyanga, alielezwa kufuzu vipimo ndani ya Klabu ya Azam FC ambayo ipo chini ya Kocha Mkuu, Mromania Aristica Cioaba, na alitarajiwa kumaliza taratibu zote za kuingia mkataba na 'Wanalambalamba' hao.

**Msimu uliomalizika wa 2019-20, akiwa chini ya kocha Juma Mgunda Lyanga aliifungia Coastal Union mabao nane.**

Kwa upande wa Niyonzima aliyekuwa akicheza Rayon Sports ya Rwanda, Azam FC imesema usajili wake ni sehemu ya mapendekezo ya benchi la ufundi la klabu hiyo.

Kiungo huyo nyota, yupo kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Rwanda 'Amavubi' na alisaini mkataba Jumamosi mbele ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat'.

Dirisha la usajili Ligi Kuu Bara, Ligi Daraja la Kwanza na la Pili, lilifunguliwa rasmi Jumamosi Agosti Mosi na linatarajiwa kufungwa mwishoni mwa mwezi huu kabla ya ligi hizo kuanza katikati mwezi ujao.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' (kushoto), akimtambulisha na kumkabidhi jezi kiungo mshambuliaji mpya, Mnyarwanda Ally Niyonzima, baada ya juzi kusaini mkataba wa miaka miwili kuitumikia klabu hiyo akitokea Rayon Sports ya Rwanda. **NA MPIGAPICHA WETU**




Kocha wa Singida United, Ramadhan Nswanzurimo

# *Tatu zapanda Ligi Kuu, tano zashuka*

**Na Adam Fungamwango**

KAZI ya kupandisha timu Ligi Kuu Tanzania Bara na kuzishusha imekamilika juzi, Jumapili baada ya jumla timu tano kushuka, huku tatu mpya ambazo hazijawahi kuwapo kwenye ligi hiyo zikipanda.

Timu zilizoshuka rasmi sasa ni Singida United ya Singida, Ndanda FC ya Mtwara, Lipuli ya Iringa, Alliance FC na Mbao za Mwanza, ambayo pamoja na kushinda mabao 4-2 nyumbani dhidi ya Ihefu FC ya Mbarali, ilijikuta ikishuka hadi daraja kwa kanuni ya bao la ugenini, kwani kwenye mechi ya kwanza ikiwa Mbarali ilichapwa mabao 2-0, hivyo matokeo ya jumla kuwa 4-4.

Timu za Singida, Alliance FC, Ndanda FC, na Lipuli zikishuka moja kwa moja baada ya kushika nafasi nne za mwisho, lakini Mbao FC ilifia kwenye mechi ya mchujo.

Timu tatu zilizopanda na ambazo msimu ujao wa Ligi Kuu zitaonekana kwa mara ya kwanza ni Dodoma Mji iliyopanda moja kwa moja kutoka Kundi A kwenye Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara, na Gwambina FC, ambayo ilikuwa timu ya kwanza kabisa kupanda Ligi Kuu, ikiwa kinara wa Kundi B.

Kwa mara ya kwanza tangu mfumo wa kucheza mechi za mchujo kuanza msimu uliopita, timu ya Ihefu FC kutoka Ligi Daraja la Kwanza imeweza kupenya kwa kuondoa timu ya Ligi Kuu huku Geita Gold ilishindwa kufanya hivyo, baada ya kufungwa jumla ya mabao 2-1 dhidi ya Mbeya City, baada ya sare ya bao 1-1 nyumbani, lakini ikafungwa 1-0 Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya Jumapili iliyopita.

# Michezo

Jumatatu Agosti 3, 2020

Nipashe




'Nafurahia FA tu, sijui hatima yangu'

UKURASA 22

MWAKA WETU TENA...




Nahodha wa Simba, John Bocco akinyanyua Kombe la FA juu huku wakisherehekea na wachezaji wenzake baada ya kulitwaa kwa kuifunga Namungo FC mabao 2-1 kwenye mechi ya fainali iliyopigwa katika Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga Mjini jana. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

## Klabu Ligi Kuu Bara kupewa fungu Fifa

**Na Mwandishi Wetu,** RUKWA

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limesema sasa rasmi litaanza kutoa mgawo wa fedha zinazotoka Shirikisho la Mpira wa Miguu duniani (Fifa), kwa wanachama wake mbalimbali ikiwamo klabu za Ligi Kuu Bara ili kusaidia shughuli mbalimbali za maendeleo.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa kikao cha Kamati ya Utendaji ya TFF jana, Rais wa shirikisho hilo, Wallace Karia alisema mgawo huo utakwenda pia mikoa yote 26 ya Tanzania Bara na mitano iliyoko Zanzibar.

Karia alisema pia fedha hizo za Fifa zitagawiwa kwa klabu za Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili, Ligi Kuu ya Wanawake na vyama shiriki vyote vinavyotambuliwa na TFF.

Kiongozi huyo alisema kikao hicho kilichofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa kimeridhia kuanza kwa ujenzi wa vituo vya maendeleo ya soka katika maeneo ya Kigamboni jijini Dar es Salaam na Tanga.

Alisema pia kikao hicho kimeridhia kuwapa mikataba mipya ya ajira kwa watendaji wake akiwamo Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, Mkurugenzi wa Ufundi, Oscar Mirambo na Mkurugenzi wa Mashindano, Salum Madadi baada ya kuridhishwa na utendaji wao wa kazi kwa miaka miwili iliyopita.

Kidao alisema anafurahi kuona shirikisho limeendelea kumwamini katika nafasi hiyo na akaahidi ataendelea kutekeleza vema majukumu yake na kulifanya soka la Tanzania kung'ara zaidi kimataifa.

# NI SIMBA YA KIBINGWA

## Makombe yote yatua Msimbazi, Chama, Miquissone walamba tuzo, Namungo chali TFF yazihamishia Arusha...

**Na Somoe Ng'itu,** RUKWA

HII ni Simba ya makombe! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na 'Wekundu wa Msimbazi' hao kukamilisha msimu wa 2019/20 kibingwa zaidi kwa kunyakua ubingwa wa tatu baada ya kuifunga Namungo FC mabao 2-1 katika mchezo wa fainali wa Kombe la FA uliopigwa jana kwenye Uwanja wa Nelson Mandela ulioko Sumbawanga Mjini.

**Hilo ni kombe la tatu msimu huu kwa Simba la kwanza likiwa ni Ngao ya Jamii ambalo walilichukua baada ya kuifunga Azam FC walipokuwa chini ya Kocha Mkuu, Mbelgiji Patrick Aussems na pia ikiwa chini ya Sven Vandenbroeck ilifanikiwa kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania kwa mara ya tatu mfululizo.**

Simba ilikabidhiwa kombe la ubingwa na mgeni rasmi, Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, aliyeongozana na mwenyeji wake, Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Leodegar Tenga na Naibu Spika, Tulia Ackson.

Licha ya Namungo kupoteza mchezo huo, tayari ilishakata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, huku Simba ikienda kupeperusha bendera ya Tanzania Bara kwenye michuano mikubwa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mabingwa Simba walienda mapumziko wakiwa mbele kwa mabao 2-0 ambayo yaliwafanya kushangiliwa zaidi na mashabiki wao waliojaza uwanja huo.

Bao la kwanza la Simba lilifungwa na Luis Miquissone ambaye alimalizia mpira uliookolewa na beki wa Namungo na kupiga shuti lililomshinda golikipa Nourdine Barola kudaka dakika ya 27 huku nahodha John Bocco akifunga la pili kwa kichwa akimalizia mpira uliotemwa.

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi kwa pande zote mbili kushambuliana kwa zamu huku wachezaji wakitumia nguvu zaidi kuliko ufundi. Dakika ya 56 Namungo ilipata bao la kwanza kupitia kwa Edward Manyama aliyefunga kwa kichwa akiunganisha mpira wa kona uliopigwa na Abeid Athumani na kuwafanya wachezaji wa timu hiyo ya mkoani Lindi 'kuamka' na kuendelea kulishambulia lango la Simba.

Simba ilikaribia kupata bao lingine dakika ya 67 kupitia Bocco, lakini mpira alioupokea kutoka kwa Miquissone na kumpiga kanzu Barola ulitoka nje huku mashabiki wakiamini wamepata goli lingine katika mchezo huo uliochezeshwa na refa, Abdallah Mwinyimkuu kutoka mkoani Singida.

Kipa Barola aliinyima Simba bao baada ya kudaka shuti la Miquissone dakika ya tisa huku Blaise Bigirimana akiokoa shuti la Clatous Chama lililokuwa linaelekea katika lango la Namungo dakika ya 16 wakati mpira wa kichwa uliopigwa na Jonas Mkude ukigonga mwamba na kutoka nje dakika ya 18.

Wakati huo huo, Miquissone alitangazwa kuwa Mchezaji Bora wa mechi hiyo ya fainali na kupokea zawadi ya Sh. 500,000 kutoka kwa benki ya KCB ambao ni mmoja wa wadhamini wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Chama alitangazwa kuwa Mchezaji Bora wa mashindano hayo msimu huu wakati Omary Yassin wa Panama FC ambaye alifunga mabao tisa ndiye Mfungaji Bora wa michuano hiyo ambayo ni maalumu kwa kusaka tiketi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba na Namungo zitakutana tena katika mechi ya Ngao ya Jamii ya ufunguzi wa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2020/21 itakayochezwa baadaye mwaka huu katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Namungo; Nourdine Barola, Rogers Gabriel, Edward Manyama, Steven Duah, Karlos Protas, Hamisi Khalifa, Hashim Manyanya/ Frank Mkumbo (dk 60), Daniel Joram/ Steve Nziamasabo ( do 46), Blaise Bigirimana, Lucas Kikoti na Abeid Athumani.

Simba ; Aishi Manula, Shomary Kapombe, Mohammed Hussein, Kennedy Juma, Paschal Wawa, Jonas Mkude, Luis Miquissone, Gerson Fraga, John Bocco, Clatous Chama na Francis Kahata/ Hassan Dilunga ( dk 26).

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >